# *Kile Kipeo*

Hebu tuviinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi. Huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa mbele za Mungu, na—nashangaa ni wangapi walio humu ndani wenye haja ambayo wangemtaka Mungu aikumbuke kwa kuinua tu mikono yenu? Sasa, shikilia haja yako moyoni mwako sasa tunapoomba.

2 Bwana Yesu, Ewe Che—Chemchemi, Chemchemi isiyokauka ya Uzima, tiririka ndani yetu leo, Bwana, na ututakase na kutokuamini kwote na dhambi yote, tupate kusimama katika Uwepo Wako sasa, tukijua ya kwamba kuna haja miongoni mwetu, ambazo tunajua ya kwamba sisi ni wenye dhambi na hatu—hatustahili baraka yo yote. Lakini basi, tunapowazia kuhusu Yeye aliyekuja na kuzichukua dhambi zetu, basi wakati Damu Yake ipo, siyo—siyo sisi katika Uwepo wa Mungu, ni Yeye—sauti yetu tu kupitia katika Damu Yake; Damu Yake inanena. Ee, Mungu, basi itakase mioyo yetu na dhambi na kutokuamini.

3 Tupe haja za mioyo yetu, kwa kuwa kweli tuna shauku hizi za kukutumikia. Katika hali hizi za unyonge na mateso na mambo ya ulimwengu tunayoletewa wakati mwingine kutukamilisha, tumeambiwa hayo, ya kwamba Yeye alisema, "Msione kuwa ni ajabu kwamba majaribu haya huwajia." Yote hutenda kazi tu kwa manufaa yetu na kwa kutukamilisha na kutuleta mpaka mahali hapo. Majangwa haya makubwa ya ujuzi, ambamo wenye haki hufanywa watakatifu, tu—tunakushukuru Wewe kwa ujuzi huu, Bwana. Hatungethubutu, hatungetaka kutenda lo lote kinyume cha mapenzi Yako; bali tunaomba, Baba, ya kwamba katika hili tutaletwa karibu na Wewe.

4 Na wakati mizigo inakuwa mizito sana hatuwezi kuendelea mbele tena, ndipo tunainua mikono yetu na kumlilia Baba yetu. Basi sikia kutoka Mbinguni, Bwana.

Tuponye. Tupe afya kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

Bariki Neno Lako asubuhi ya leo, Bwana. Neno Lako ni Kweli.

5 Nasi tunakutanika hapa sasa kanisani. Tunamwombea Ndugu Neville, na Ndugu Capps, na Ndugu Collins, na wahudumu wengine wote, na—na wadhamini, mashemasi, na wafuasi wote, na wageni malangoni mwetu. Hebu na hii iwe siku ambayo tutaikumbuka kwa muda mrefu kwa ajili ya Uwepo Wako.

6 Tuko hapa chini ya matumaini makuu asubuhi ya leo, Bwana. Kwa tangazo la muda kidogo sana, tumekutanishwa.

Tunaona ya kwamba ni kwa kusudi fulani. Hebu na kusudi Lako litimizwe, Bwana. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake Yesu, tunapojitoa wenyewe. Amina.

7 Ni heshima sana kuwa hapa na kukutanika pamoja na kanisa hili lililojaa watu. Sikuwa nikitarajia kuwa—hata mtu mmoja asubuhi ya leo, kwa kuwa hata mimi sikujua nitakuwa hapa.

8 Tumekuja hivi punde kutoka Philadelphia. Na hivyo nilikuja nikitarajia kwenda Arizona upesi sana kwa—kufanya ibada ya mazishi ya rafiki yangu, Kapiteni Jim Mosely, kijana wa thamani sana, na mcha Mungu niliyemwongoza kwa Kristo si muda mrefu uliopita, wale ndugu watatu wa Mosely. Na mmoja wao alianguka kisha—kwa ndege hivi majuzi akafa papo hapo. Alilala motoni masaa kumi kabla hawajamfikia. Kwa hivyo aliwaacha . . . ana umri wa miaka ishirini na minane, mkewe ishirini na sita, na—na amewaacha watoto watatu—wa kwanza ana miaka saba. Huzuni mno. Nao . . . Walipomleta mle, basi iliwapasa kumzika siku iliyofuata. Kwa hiyo mimi tu—mimi sikuweza kwenda. Nami niliandika tu—ama nikatuma habari kwa simu yale ningesema, ama yale ningalisema kwenye mazishi ya Ndugu Mosely. Baadhi ya mambo haya hatuwezi kuyafahamu, bali hata hivyo Yeye hufanya kila kitu kitendeke barabara kabisa.

9 Tuko hapa katika utumishi wa Bwana asubuhi ya leo, tukijua ya—ya—ya kwamba tunamwamini Mungu, ya kwamba tunaamini kwamba atafanya kila kitu sawa kabisa. Haidhuru ni nini na jinsi itakavyokuwa, tunajua sharti iwe na manufaa. Yeye aliahidi hivyo. Haina budi kuwa hivyo. Wakati mwingine hatuwezi kufahamu hilo, huwa gumu sana wakati mwingine, hata hivyo tunajua ya kwamba ni kweli, maana Biblia inasema ni Kweli. Na Biblia kwetu ni Mungu katika andiko.

10 Sasa, hatuna budi kuweka imani yetu mahali fulani. Na kama—kama mimi—mmoja wetu maishani alijaribu kujifanikisha maishani hata akawa zaidi ya milionea mara nyingi . . . Lakini tutafanyaje na hayo? Hatuna budi kufika mwishoni mwa safari yetu na—na ina faida gani kwetu wakati huo? Mnaona? Na pesa ni—ni hati, ni kitu cha kubadilishana; lakini hauwezi kuibadilisha kwa Uzima. Mungu ndiye pekee aliye na Uzima.

11 Kwa hiyo tu—tunatambua ya kwamba tuko hapa katika hali ya kivuli. Na mradi tu kuna kivuli, lazima kuwe na kilicho halisi. Haiwezekani kuwepo na kivuli pasiwepo kilicho halisi (waona?), kwa maana kivuli hufanyizwa kwa kitu halisi. Kwa mfano kama ulikuwa na negativu ya picha ya kitu fulani. Sharti pawe na kitu mahali fulani ama—kugusa nuru—kugusa hiyo lenzi ama hapatakuwepo na—na negativu yo yote. Kwa hiyo tunapoona ya kwamba maisha yetu hapa ni kivuli na tukijua kwamba tuko katika mfano wa uhai fulani mahali fulani, ndipo basi tunajua

ya kwamba kuna kitu halisi mahali fulani ambacho hiyo nuru imekigusa, nayo inarudisha mng'ao wake hapa duniani. Nasi ni mng'ao huo tu. Kile kitu kilicho halisi kiko mahali fulani. Kama hivyo sivyo, mimi ni mtu aliyedanganyika sana ulimwenguni; nimetumia maisha yangu bure. Bali najua yakini kwamba kiko! Mnaona? Na hiyo ndiyo sababu tuko hapa.

12 Ninapowaona ninyi watu mkija humu kutoka kila mahali nchini kwa tangazo la ghafla, na wakati mwingine ni kwa kudhania tu, basi inanifanya nijisikie duni sana ninapokuja katika mkutano kama huu, nikiwazia ya kwamba najua watu hapa wamesafiri kwa mamia ya maili wapate tu kuwa hapa kwa ajili ya dakika chache za ibada, kuketi hapa tu.

13 Mwanamke fulani alitoa matamshi, akaja hivi majuzi akasema, "Nionyeshe mahali mtu huyo alipotembea, kisha nitatembea nyuma yake ardhini," kasema, "nitapata afya." Sasa, watu wanakuamini hivyo, nawe ni mwakilishi wa Kristo, basi tufanyeje? Yatupasa tujihadhari sana, kwa sababu hujiangamizi tu kwa makosa, unawaangamiza wengine wanaokufuata.

14 Kwa hiyo sijui dhehebu lo lote ama cho chote kile nikupeleke humo. Kuna jambo moja tu ninaloliamini (kama unaniamini, yafuate ninayokwambia, kwa sababu ninaamini Biblia), hilo ni Neno la Mungu. Mambo mengine hushindwa. Mimi . . . Yeye ni Uzima. Yeye ni Neno.

15 Sasa, najua ya kwamba ninyi . . . Ninapokuja hapa mimi huwachelewesha sana. Nilimuomba Mungu nilipojisikia kama nataka kuja hapa leo . . . Nimekuwa na mahojiano mengi, na simu, na kadhalika; ilinipasa kukutana na baadhi yao asubuhi ya leo. Nami nikasema, "Vema, Ndugu Neville hapana shaka ataniomba nizungumze." Hiyo ilikuwa Ijumaa. Nami nikasema, "Ndugu Neville huenda akaniomba kuzungumza. Na nitakapofanya hivyo, ndipo naomba, Mungu . . . " Kuna joto sana, imekuwa joto sana. Na Yeye amekuwa mwema akatutumia mvua na kukatiza joto lililozidi sana na kutupa asubuhi njema asubuhi hii. Naomba ya kwamba wema Wake utamtiririkia kila mmoja wenu hata mtakumbuka daima kuwa mlikuwa hapa asubuhi hii. Neema Yake na baraka Zake ziwe juu yenu.

16 Usiku wa jana nilimtembelea rafiki aliye mgonjwa, Ndugu Bill Dauch. Simwoni humu asubuhi ya leo. Sijui kwa nini mimi . . . Lo, huyu hapa. Naam. Nami nilikuwa nikiwazia: "Mzee wa miaka tisini na mmoja na angali anatembea kishujaa humu—humu nchini, kuvuka majangwa, na kuvuka milima yenye theluji, na barabara zenye kuteleza. Si lazima afanye hivyo. Mungu amekuwa mwema kwake; si lazima afanye hivyo. Angekaa nyumbani na watumishi wampepee kama angalitaka." Lakini jambo fulani lilimpata Bill Dauch; alizaliwa mara ya pili. Na hiyo ilipotukia, kitu fulani kikaingia moyoni mwake, hata ikawa kusudi lake la kuishi ni kuhudhuria ibada hizi.

Kisha, kama nitakuwa mnenaji wa Mungu, je ningalimdanganya rafiki? Afadhali nife. Basi hebu nimwambie hasa yaliyo Kweli kutoka Biblia hii. Ndipo hilo ndilo Neno la Mungu. Ninarudia tu aliyosema Yeye.

17 Sasa, nataka kusoma kidogo Biblia. Na kabla hatujasoma, ningetaka ku—kusema ya kwamba naamini usiku wa leo ni usiku wa Ushirika. Nanyi mnao—mnaotoka mahali hapa (bila shaka hao watu wengine labda watarudi makwao, maana hawana budi kwenda kazini)—ninyi mnaotoka mahali hapa katika kusanyiko hili, kumbukeni, ndugu watawahudumia Ushirika usiku huu.

18 Sasa, ninangojea wi—wito wa mwisho kwenda Africa. Hawange—hawangenikubalia niende kama mishenari. Kwa hiyo njia pekee ninayoweza kwenda, huko. . . Ninakwenda Kenya, Uganda, na—na Tanganyika. Na njia pekee ninayoweza kwenda huko. . . Kwanza, makanisa hayatakuruhusu kuingia, maana wao wanataka nihubiri jambo fulani upande huu na upande *ule,* kule Afrika. Nami sitaenda huko hivyo. Nisingekuwa mnafiki wa kutosha kufanya hivyo. Kwa hiyo aidha niwaambie, "La bwana, nitahubiri yale tu Mungu anayoweka moyoni mwangu na hayo tu." Waona? Nami nina hakika hayatakuwa yale wanayojaribu kunifanya nifundishe. Kwa hiyo—ubatizo wa utatu, na kadhalika namna hiyo, na kubishana nao. La!

19 Lakini nimealikwa kwenye mkutano mkubwa na Ndugu Boze. Yeye yuko karibu sana kuona nuru ya yale tunayoamini. Kwa hiyo nimeomba niende kule kana kwamba nakwenda katika ziara ya kuwinda. Wakiniruhusu niingie, kama kwenda kuwinda. . . Kama nikimpata mtu kusema wangenipeleka nikawinde, ndipo nitakapoingia kule (daktari—daktari aliyeko kwenye ubalozi ni rafiki yangu kutoka Chicago)—na mara nitakapoingia kule, yeye atasema, "Vema, huyu hapa Ndugu Branham huku. Hebu na tufanye mkutano." Kwa hiyo baada ya kufika huko ubalozi hauwezi kunikataza. Kama wao. . . Hivyo wao wanajaribu kushughulikia jambo hilo sasa. Kwa hiyo nasadiki ya kwamba. . . Kama ni mapenzi ya Mungu itakuwa hivyo. Mwaona? Hili—hili limekabidhiwa Kwake. Kama sivyo, basi nitawajulisha.

20 Nataka. . . Yakiwa ni mapenzi ya Mungu basi, nataka kuhubiri juu ya zile Baragumu Saba. Na hiyo itakuwa ibada ya kama siku nane. Nasi hatutakuwa hapa maskanini; labda tutajaribu kupata ukumbi fulani hapa.

21 Sasa, sikufikiria juu ya ukumbi huu mpya unaojengwa hapa. Ni mahali pale hasa nilipomwona Yesu mara ya kwanza katika ono (sasa, ni—ukumbi huo umejengwa juu ya mahali papo hapo. Nilikwenda pale hivi majuzi kuangalia), nilipomtazama na kumwona Yeye akiangalia upande wa mashariki (mnakumbuka mmenisikia nikisimulia hayo), nilipokuwa kule nikimwombea baba yangu, nikiwa—nikiwa kijana mdogo, mhubiri kijana tu.

Hapo ndipo nilipomwona Yeye, amepiga hatua, nikimtazama Yeye. Kichwa Chake kiliangalia kando ya pale nilipokuwa. Niliendelea kutembea, nikikohoa, katika uwanja wa majani. Nami nikaendelea kuangalia, na Yeye hakugeuka. Nikaliita Jina Lake, Yesu, na Yeye aligeuka, akainua mikono Yake. Na hayo tu ndiyo niliyokumbuka mpaka mapambazuko. Ndipo nikatoka huko uwanjani karibu mapambazuko. Kwa hiyo basi labda Bwana ataniruhusu kuhubiria mle hizo Baragumu. Popote pale, mapenzi ya Mungu yakatendeke.

22 Fungueni Biblia zenu sasa katika Isaya 50—sura ya 53 ya Isaya. Sasa, tunasadiki ya kwamba Mungu atabariki jitihada zetu dhaifu za kukutanika pamoja asubuhi ya leo. Tumetoka Philadelphia hivi punde, ambako nilikuwa kwenye mkutano wa Wafanyi Biashara Wakristo wa Injili Yote. Na katika kusikiliza shuhuda zao mbalimbali na kadhalika kule. . .

23 Kisha nami—nilipokuwa nikija. . .Billy Paul, pamoja nami, na Rebeka, na msichana mdogo wa Collins, kitoto Betty Collins. . .Naye Billy anapenda kulala sana, na Becky ni zaidi. Na kwa hiyo mimi—Mimi na Betty tulikuwa tukizungumza. Naye alikuwa ameketi kule nyuma pamoja na Becky katika kiti cha nyuma. Nami nikaona kitu fulani kikitendeka barabarani. Na nilipoona, kitu fulani kikanijia. Naye Betty (kama yuko hapa), aliona kwamba nilinyamaza nikaanza kuandika jambo fulani. Hapo ndipo nilipopata somo hili la asubuhi hii.

24 Sasa, hebuni na tusimame kwa miguu yetu kama sisi. . . Sasa, sisi husimama kwa kuliheshimu Neno la Mungu, ninaposoma Isaya sura ya 53:

> *Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa Bwana umefunuliwa nani?* (Tazama, kwanza ni swali.)
>
> *Maana alikua mbele zake kama mche mwororo, Na kama mzizi katika. . .nchi kavu; Yeye* hana *umbo wala uzuri; Na tumwonapo, hana uzuri hata tumtamani.*
>
> *Alidharauliwa na kukataliwa na* wanadamu; *Mtu wa huzuni nyingi,. . .ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao; Alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu.*
>
> *Hakika ameyachukua masikitiko yetu,* naye *Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa.*
>
> *Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu: Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; Na kwa kupigwa kwake tumepona.*
>
> *Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.*

*Alionewa, na...kuteswa, Wala hakufunua kinywa chake: Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjioni, Na kama vile kondoo...anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake; Naam, hakufunua kinywa chake.*

*Aliondolewa gerezani na hukumuni: Na maisha yake nani atakayeisimulia? Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; Alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu.*

*Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake.*

*Lakini BWANA aliridhika kumchubua;* Yeye... *amemhuzunisha; Utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi,* Naye *ataona uzao wake, ataishi siku nyingi, Na mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake;*

*Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake* Atawafanya watumishi wengi wenye haki kuhesabiwa haki...*wengi; Naye atayachukua* uovu wao.

*Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, Naye...atagawanya* nyara *pamoja na walio hodari; Kwa sababu* amemwaga *nafsi yake hata kufa, Kisha akahesabiwa pamoja na hao wakosao. Walakini alichukua* dhambi za *watu wengi, Na kuwaombea wakosaji.*

25 Baba Mungu, Neno Lako ni Taa, Nuru ambayo huangaza njia ya kila mwamini kumwingiza katika Uwepo wa Mungu, inapotupeleka kama taa mkononi mwetu. Haujatoa ya kutosha tupate kuona mwisho tangu mwanzo, na—ila mimi hutembea kwa imani. Lakini kama mtu anavyotembea katika msitu wenye giza usiku (na hapo ndipo tulipo), taa anayoishikilia humwongoza tu hatua kwa hatua. Lakini ni hiyo njia, ingawa inaelekea juu, tembea tu na hiyo Nuru. Tujalie ile Nuru iliangazie Neno leo kutuongoza hatua moja zaidi kuuendea Ufalme wa Mungu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. (Ketini.)

26 Somo ninalojisikia kuzungumza kwa makutano leo ni *Kile Kipeo*.

Laweza kuonekana jambo la kushangaza kutilia maanani kusomwa kwa—kwa Andiko kama hili la—la mojawapo ya matukio ya Biblia ya machubuko sana na ya mauaji sana, ambapo Biblia inasema kwamba huyu mtumishi Mkamilifu aliyeteswa, na akachubuliwa na kuraruliwa, na hata hivyo kutoa somo hapo kama *Kipeo*. Ajabu sana.

27 Lakini mimi—mawazo yangu yanawazia asubuhi hii tunaporudi nyuma (mimi nafanya hivyo) kwa miaka michache. Nilialikwa kwenda Forest Lawn kule—kule California upande wa juu wa Los Angeles. Kusudi langu la kwanza kwenda huko lilikuwa kuzuru ka—kaburi la—la Aimee Semple MacPherson, mwanzilishi wa shirika la Foursquare. Nami nikazuru kaburi la—lake. Nami. . .Ingawa si—sikubaliani na mwanamke huyo kama mhudumu, hata hivyo mimi—moyoni mwangu ninampenda na kumheshimu kwa—kwa ajili ya yale aliyoshindania katika ile—ile saa na mateso na mambo aliyopitia katika—katika wakati wake hapa duniani. Halafu, kwa ajili ya mwanawe mpenzi, aliye rafiki msiri wangu, Rolf McPherson.

28 Na kundi la wahudumu, tukaenda kule. Nao—hatukupata wakati wa kuingia—kuingia—mahali wachomeapo maiti na kuiweka ile—ile miili katika ki—kijisanduku kidogo ukutani.

29 Na huko wana vitu vya maana sana kama ile Meza ya Bwana ya Mwisho. Nako kunaangazwa na nuru halisi ya jua. Nao wana—wana dirisha linalowapa. . .Wanapoingia, kuna nuru; kisha wanapoanza kuzungumza giza linaanza kuingia. Na baada ya kitambo kidogo mahali pote panakuwa giza. Ndipo watu wanaondoka.

30 Nao wana hiyo Meza ya Bwana. . .Na yule mwanamke aliyekuwa na hiyo siri ya jinsi ya kufua kioo hiki kukiingiza mahali hapa, hata, kuchora hizi picha, kumbe, ili—ilipitia katika ukoo mmoja tangu miaka mingi iliyopita. Na ujuzi huo walipewa tu watoto, na wa mwisho alikuwa mwanamke. Nao walikuwa wakiichora picha hii. Nao walipoanza kukifinyanga na kukichoma moto kile—kile kioo, kukikausha, cha Yuda Iskariote, kikapasuka. Kwa hiyo basi, wakajaribu tena. Nacho kikapasuka tena. Naye akasema, "Labda Bwana wetu hataki picha ya adui Wake iwe karibu Naye." Kisha akasema, "Kama kikipasuka tena, hatutaimaliza picha." Lakini hakikupasuka wakati huo. Halafu. . .Bila shaka hilo lilikuwa jambo la kushangaza, na jinsi jambo kama hilo lingetendeka.

31 Lakini basi, moja ya mambo muhimu yanayonivutia katika Forest Lawn ni ile ya Michelangelo, ile sanamu kubwa, ile—ile sanamu ya Musa. Hiyo ni—ni nakala yake, bila shaka. Si ile ya kwanza. Lakini ilikuwa ni—ni kipeo kikuu. Na niliposimama nikaiangalia, mimi—mimi niliipenda, kitu kinachoonekana kama kwamba ni—kinawakilisha, kina jambo fulani.

32 Napenda sana sanaa. Naamini Mungu yumo katika sanaa. Naamini Mungu yumo katika muziki. Naamini Mungu yumo katika maumbile. Mungu yupo kila mahali. Na cho chote kilicho kinyume cha asili ni upotovu. Mungu yumo katika dansi, si aina ya dansi mnayocheza hapa, lakini wakati wana na binti za Mungu wamo katika Roho wa Mungu (mwaona?), huko ndiko kucheza dansi. Lakini kama iliyonilazimu kushindana nayo

hata saa 8 usiku wa kuamkia leo juu kule kinjiani, hiyo ndiyo upotovu wake.

33 Lakini hii. . . Katika kile kipeo ambacho Michelangelo alikuwa—alikuwa ametengeneza, ili—ilimgharimu kitu fulani kufanya hivyo. Huyo. . . Yeye alikuwa mtu mashuhuri. Nayo ilimgharimu sehemu kubwa ya maisha yake, kwa sababu alitumia miaka mingi, mingi sana akiichonga. . . Kuchukua tu jiwe na—la—la marmar na kuendelea kulichonga. Na kuona. . . Ni mtu huyo tu, fundi wa kuchora mawe, aliye na yale akilini mwake anayotaka kufanya; ndiye—ndiye pekee. Waweza kumwendea na kumwambia, "Kwa nini unachonga-chonga huo mwamba?" Kwa mgeni asiyejua kilicho moyoni mwake, ni upuzi. Bali kwa mtu huyo, mchongaji mwenyewe, ana—ana pi—picha akilini mwake, ya kile anachojaribu kutengeneza, naye anajaribu kufanyiza kilicho akilini mwake katika mfano wa—wa sanamu ya ukumbusho. Na hiyo ndiyo sababu anaichimbua toka miambani.

34 Na kufanya hivi, sharti uanzie mwanzoni, na sharti ufuate kielelezo. Waona? Huwezi kuchukua kipande kidogo kuaza: "Tutaitengeneza hivi. La, naamini. . ." La, hana budi kupata kielelezo halisi. Na akilini mwake ana kielelezo hicho. Naye hawezi kubadili kielelezo hicho. Sasa, ili kufanya hivi ilimpasa kuchora akilini mwake (kwa sababu hatuna picha halisi za Musa)—bali ilimpasa kupata taswira akilini mwake ya jinsi Musa alivyokuwa hasa.

35 Sasa, fundi halisi wa kuchonga ana uvuvio, kama alivyo mshairi ama mwimbaji ye yote wa kweli, mwana muziki, ama ye yote yule. Yote yaliyo halisi hayana budi kuja kwa uvuvio. Michelangelo hana budi alipata uvuvio wa jinsi Musa alivyokuwa, naye akashika akilini mwake jinsi Musa alivyokuwa. Kwa hiyo akaanza kazi kwa kipande hiki kikubwa cha marmar kukikata kulingana na ule mfano, na kukichonga, kukisugua, hata akafikia ile picha halisi ya kile kilipaswa kuwa akilini mwake.

36 Kisha alipoikamilisha yote, kila kona imenyoshwa, na kila mahali pamesuguliwa, na macho sawa kabisa, na kila unywele na ndevu, zote jinsi zilivyokuwa, alisimama kando akaiangalia. Na—nawazia ile—ile miaka mingi, mingi sana ya kazi ngumu, na jinsi ilimpasa kushikilia picha ile wakati wote akilini mwake ya yale angefanya. Na fikiria tu, picha hiyo akilini mwake kwa miaka mingi sana, kuifanya ionekane jinsi ilivyokuwa hasa—aliipata hiyo picha kwanza—na jinsi ilivyompasa kufanya kazi kwa picha hiyo, akichonga-chonga na kutengeneza. . . Na alipoikamilisha kabisa, hata ikawa kamili hasa, alisimama akaiangalia alipoimaliza asubuhi hiyo, huku ameshika nyundo. Naye alivuviwa sana alipoiangalia, kwa kuwa picha ya moyo wake ilikuwa imesimama mbele yake ikiwa katika hali halisi. Kile alichokuwa ameona na yale—mawazo yake juu ya sura ya

Musa, kilikuwa kimesimama mbele yake, kile alichokuwa nacho moyoni mwake miaka hii yote ya kazi ngumu, na masaa kadha ya huzuni, na dhiki, na watoa lawama, na kila kitu, lakini hata hivyo yeye alidumu tu na lile ono hata lilipotimizwa.

37 Na wakati ilipokwisha timizwa, alisimama kando huku ameshika nyundo (nyundo ya mchoraji) mkononi mwake, naye akaiangalia hiyo sanamu. Na uvuvio wa ile taswira, ambayo alikuwa ameiona ya jinsi ya kutenda hayo, ukamvuvia sana hata yeye—uvuvio ukamshika sana hata hakuweza kujizuia na akaipiga gotini na kusema, "Nena!"

38 Na sasa kuna waa katika hiyo sanamu mashuhuri, gotini, kwenye goti la kuume. Mahali hapo ni yapata inchi sita juu kidogo ya goti. Niliingiza mkono wangu pale, kina chake *hivi*.

39 Baada ya kutumia wakati huo wote, kwa miaka kadha wa kadha kuitengeneza hii, halafu kwa—kwa ushawishi wa kuona kile alichokuwa ameona moyoni mwake na katika ile picha kimetimizwa, na alichotaka sana kuona, kimekamilishwa. Na wakati kilipokamilishwa, alivuviwa sana nayo hata akafikiri kipeo chake kinapaswa kumzungumzia. Naye akakipiga mguuni na kupaza sauti, "Nena!" Nayo ikapata waa. Hiyo sanamu ikapata waa.

40 Kwangu mimi, hilo waa ndilo lililoifanya kuwa kipeo. Sasa, labda kwa—kwa akili inayoweza kuwazia vinginevyo, unafikiri hilo liliiharibu. La, kwangu mimi li—liliifanya jinsi ilivyokuwa. Hiyo—hiyo. . .Kwa maana baada ya miaka mingi sana ya kazi ya ustadi, uchovu, na uvuvio, na kadhalika katika kuitengeneza, jitihada zake zilikuwa zimethibitisha hazikuwa za bure—ilikuwa kamilifu, na hiyo ndiyo sababu yeye alipaza sauti, "Nena!" Kwa sababu alikuwa ameona mbele yake ya kwamba alikuwa—alikuwa amefaulu, kutimiza picha iliyokuwa akilini mwake; na kwa hiyo, kwa uvuvio alifanya jambo fulani bila kufikiria, lisilo la kawaida; aliipiga na kusema kwa sauti kuu, "Nena!" Waona, hangalifanya hivyo kama angefikiri. Lakini hakufikiri. Ilikuwa uvuvio wa kuona kile kilichokuwa moyoni mwake kimekaa pale kikamilifu mbele zake.

41 Jitihada zake, na uchovu wake, kazi za usiku, na kutengwa na ulimwengu kwa siku kadha. . .Na labda anakula sambusa moja, na—na kuisugua, kisha anarudi na, "Sasa, hivyo sivyo ilivyokuwa. Sasa, haina budi kuwa hivi," na kuisugua. . .Ndipo alipoiona imekamilika kabisa, ndipo akaiona katika hali yake halisi. Ile negativu ya—kile kilichokuwa akilini mwake kilikuwa kimekuwa halisi; kikawa kitu dhahili; kwa hiyo, kikamjia ghafla. Na ilikuwa halisi mno hata akawa hana budi kusema kwa sauti kuu, "Nena!"

42 Kwangu mimi ilikuwa kurudishwa kwa sura, ilikuwa—ilikuwa ni sifa ya kazi yake, kwamba kazi yake ilimvuvia sana hata hakuweza kujizuia kuipiga na kusema, "Nena!"

43 Nilisimama hapo nikaangalia sanamu hiyo. Nikawazia juu ya masaa ambayo mtu huyo alikuwa hana budi aliyatumia katika kuitengeneza. Nao wakasema ilikuwa miaka mingapi. Lakini ilikuwa—ilikuwa kurudishwa kwa sura iliyokuwa akilini mwake, kwa sababu ilikuwa msaada kwa—kwa sanaa yake mashuhuri, kazi yake kuu aliyokuwa akifanya. Na hatimaye alipofaulu, ilikuwa kazi kubwa sana.

44 Sasa, hebu tugeuze ukurasa wa Michelangelo kisha tukifunge kitabu. Na hebu tukifungue Kitabu kingine nasi tusome habari za Fundi Mchongaji Mkuu, Mwenyezi, ambaye kabla ulimwengu haujakuwapo na kabla misingi haijawekwa, yale aliyotaka Mwenyewe yalikuwa mawazoni Mwake. Na Yeye alitaka kumfanya mtu katika mfano Wake. Alitaka kutengeneza kitu ha—halisi cha kile kilichokuwa ono Kwake, kile kilichokuwa mawazoni Mwake.

45 Sasa, kwa Michelangelo hicho kilikuwa sifa ya wazo lake. Naye Mungu alitaka kumfanya mtu kwa mfano Wake—yule Mchongaji Mkuu—na Yeye akaanza kumtengeneza. Nasi tunaona Yeye alipoanza kutoa kutoka kwa vitu vinavyoonekana, cha kwanza labda kilikuwa samaki, halafu ndege, na—halafu viumbe vitambaavyo juu ya uso wa nchi, na vitu vingi Yeye alivyoleta. Lakini hatimaye alipokuwa akiatamia, akiwa Muumba, Yeye alikuwa...Hakuwa kama mwanadamu sasa, fundi mchongaji ambaye hana budi kuchukua kitu ambacho tayari kimeumbwa kutengenezea sanamu. Yeye alikuwa Fundi Mchongaji wa mambo ya Milele. Yeye alikuwa Mchongaji ambaye angeweza kuumba na kukifanya kiwepo kitu kile alichokusudia mawazoni Mwake kufanya; au vinginevyo, Yeye anaweza kufanya kitu kionekane ambacho sifa Zake zilikitaka.

46 Na alipoanza kutengeneza vitu vitambaavyo, kama wa—wa—wanyama wadogo juu ya nchi...Halafu, Yeye akaanza kukifanya kutoka hicho hadi kitu kingine cha hali ya juu zaidi. Hatimaye Yeye akawaumba wanyama wakubwa kama simba, chui mkubwa, dubu. Kisha akawaleta hata katika—katika—katika maisha labda ya—ya nyani, na sokwe, na kadhalika. Sasa, si mabadiliko ya viumbe, kama tunavyofikiria ya kwamba mtu alitoka kwa..., huo ulikuwa uumbaji mkamilifu, Mungu akitenda kazi kwa utaratibu.

47 Lakini hatimaye kukatokea duniani ukamilifu, na huo ulikuwa mwanadamu. Na ndipo Yeye angeona katika mtu huyo, ya kwamba alifanana na Yeye. Hivyo sasa, wakati Yeye alipomtazama Huyo, alikuwa kurundishwa kwa sura ya jinsi Muumba wake alivyokuwa. Mungu sasa alikuwa amefaulu kupata kitu kile Yeye alichohitaji, mtu katika mfano Wake.

48 Ndipo huenda nikasema hivi: ya kwamba alipomuumba mtu huyu kuna kitu kwake ambacho hakikuonekana sawa, kwa sababu yeye—yeye alikuwa peke yake. Na hivyo ndivyo Mungu

alivyokuwa—peke Yake. Yeye alikuwa wa Milele. Na mtu huyo sasa katika mfano wa Mungu pia alikuwa peke yake duniani. Kwa hiyo Yeye hapana budi alimpiga pigo dogo katika ubavu wake wa kushoto, na kutoka hapo Yeye akakichukua kipande kilichotoka humo na kumfanyia msaidizi, mke. Ndipo basi hakuwa peke yake; alikuwa—alikuwa—alikuwa pamoja na mtu mwingine. Na hiyo ndiyo kazi Yake iliyo kuu.

49 Na Yeye, kama mchongaji stadi angechukua kipeo cha—cha—chake. . .Sasa jambo la kwanza, Yeye alikuwa na kipeo Chake Mwenyewe. Lakini sasa, Yeye aliona ya kwamba hicho kipeo kilikuwa na upweke kama Yeye alivyokuwa, hivyo akakigawanya hicho kipeo kwa kukipiga ubavuni na kumtoa msaidizi.

50 Na sasa, kuwafanya hao wawili mmoja, Yeye akawaweka, kama mchongaji ye yote stadi, mahali ambapo—ambapo ni pazuri. Fu—Fundi wa kuchonga asingechonga kipeo chake kikuu kisha akakichukua akakiweka kichochoroni mahali fulani ama kukificha nyuma ya nyumba. Kama alivyotuambia Bwana wetu, “Mtu haiwashi taa na kuiweka chini ya pishi.” Tunapofanyika vipeo vya Mungu, hatupaswi kujificha vichochoroni mahali fulani; sisi—sisi hatuna budi kutoa nuru.

51 Kwa hiyo tunaona ya kwamba—ya kwamba Yeye—baada ya Yeye kutengeneza hiki kipeo. Alikiweka hapa juu ya nchi na kukiweka mahali pazuri sana, katika bustani ya Edeni. Yeye aliweka kipeo Chake (hao wawili wakiwa mmoja) katika bustani ya Edeni. Ilimlazimu kupendezwa jinsi gani, kwamba Yeye aliona hiki kipeo kilikuwa kizuri. Yeye. . .Baada ya hayo tunaona ya kwamba Yeye alipumzika; Yeye alipendezwa sana na kazi Yake.

52 Sasa kumbukeni, ya kwamba kwa maoni yangu kile kipeo ni lile pigo lililokitia waa kipeo cha Musa katika ile sanamu iliyochongwa na San Angelo. Na lilikuwa pigo lililoukata ubavu wa kipeo Chake likamtoa bibi-arusi. Na sasa, tunawaona kama jamaa kipeo katika bustani ya Edeni. Kilikuwa kizuri sana. Nacho kilimfurahisha sana, mpaka Yeye—Yeye akapumzika wakati huo; Yeye akasema, “Nita—nitastarehe.”

53 Lakini Yeye alipokuwa anastarehe na kukitumainia kipeo Chake, adui Wake akaja akakikuta hiki kipeo kikuu; naye—kwa udanganyifu akatambaa chini ya—ya kuta za ile bustani, kisha aka—akakiharibu hiki kipeo kizuri. Ali—alikiharibu hata—hata kikaanguka.

54 Sasa, ninajaribu kuangalia ile saa. Nami nilimuuliza Mike, mpwangu, kupiga ile kengele katika muda wa dakika thelathini, lakini mimi—yeye hafanyi hivyo, nami tayari nimemaliza dakika thelathini, lakini ni—. . .Tutaendelea mbele kidogo. Mwaona? Sasa, sitaki ku—kuvunja sheria hizi; mimi—mimi niliweka hizi

sheria. Mnaona? Na mimi—mimi...Na hapa unavunja sheria zako mwenyewe.

55 Sasa tazama. Basi hiki kipeo, wakati Shetani alipokishika (yule mdanganyifu)—alipopenya kati ya zile kuta, na—na kukiharibu hiki kipeo. Kwa sababu jinsi Yeye alivyokitengeneza...Je, vipi—jinsi gani alifanya hivyo? Nitaeleza kinaganaga, jinsi alivyotenda jambo hilo, hiki kipeo kilikuwa kimezingirwa kwa Neno, Neno la Mungu. Nacho hicho kipeo chenyewe, ile jamaa, ilikuwa imezingirwa kwa hili Neno; lakini ile sehemu iliyovunjika ilipovunjika kutoka kwa kile cha asili iliruka huo ukuta hadi ng'ambo na ikampa Shetani nafasi ya kukiharibu. (Na sasa, kwa kuwa mnajua ninavyoamini juu ya mambo hayo, hivyo sitaeleza hayo.) Lakini kile kipeo kilivunjwa.

56 Bali yule Mchongaji Mkuu, wakati Yeye alipoona kule kuanguka kwa familia Yake, kile kipeo. Yeye hakutaka kukiacha kimelala hapo uso chini na katika uharibifu; papo hapo Yeye alianza kufanya kazi kukiunda tena. Hakutaka kipotee, kilale hapo hivyo wakati wote, kwa sababu Yeye ni Mungu na Yeye hatashindwa. Kwa hiyo Yeye papo hapo akaanza kufanya kazi kumjenga mtu tena katika mfano Wake.

57 Sasa, tunaona ya kwamba ule ulimwengu uliokuwapo kabla ya gharika ulikuja ukaharibu kitu hicho chote, kwa sababu yale maagano yaliyofanywa, yalifanywa kwa masharti: "Iwapo hutafanya hili au iwapo utafanya lile..." Mungu, yule Mchongaji Mkuu, aliona ya kwamba mwanadamu asingeweza—asingeweza kutunza agano. Hawezi kufanya hivyo. Hamna njia ya kufanya hivyo kamwe.

Kwenye mahojiano muda mfupi uliopita nilikuwa nikizungumza na mtu fulani chumbani aliyeko hapa sasa. Naye akasema, "Lakini Ndugu Branham, nina mambo mengi sana ambayo mimi—mimi ninajua kuwa ni makosa." (Na ni—ni maskini mwanamke mcha Mungu.)

58 Nikasema, "Lakini—lakini angalia, Dada, wewe—wewe usijiangalie mwenyewe, ni—ni kile kilicho shauku yako na kile unachojaribu kufanya. Na iwapo kweli unampenda Bwana, unajaribu kumtumikia kwa moyo wako wote. Ndipo basi makosa yako yote yamefichwa katika Damu ya Bwana Yesu. (Waona, waona?) Yeye aliiandaa njia."

59 Kwa hiyo Yeye alianza sasa, akimchukua mtu kutoka kwa maagano Yake ya—ya kusema kwamba, kama "Ukitaka kufanya, Mimi nitafanya." Na Yeye akaanza na mtu aitwaye Ibrahimu na akampa Ibrahimu agano, bila masharti. Kila wakati alipoanza kipeo, Shetani angekipata, kwa sababu ya Neno. Bali Yeye alipoanza na Ibrahimu, Yeye alisema, "Nimekwisha kufanya hivyo tayari." Sasa, hili halina masharti, siyo, nini—kwamba—kwamba, "Ukifanya hivi, Mimi nami nitafanya," lakini, "Mimi

tayari nimefanya hivyo." Sasa Yeye, yule—yule Mchongaji, ameazimia kuwa na hiki kipeo.

60 Kisha toka kwa Ibrahimu wakaja wale wazee wetu. Nao hao wazee kweli . . . Sasa, Mungu anafanya nini? Anajenga tena hiki kipeo kilichokuwa kimeanguka. Hivyo katika wale wazee wetu, wa kwanza tunaona alikuwa Ibrahimu.

61 Sasa tazama. Kila kipeo huwekwa juu ya msingi wa sanamu. Ile sanamu kubwa ya Musa iliyochongwa na Angelo iko juu ya marmar yenye urefu wa futi tatu au nne. Ina msingi. Kwa hiyo Mungu alipotayarisha hiki kipeo, Yeye alikiweka juu ya msingi wa wale wazee. Na msingi wa hao wazee, wa kwanza alikuwa Ibrahimu, kisha Isaka, halafu Yakobo, ndipo Yusufu—zile pembe nne.

62 Na sasa, Ibrahimu alikuwa msingi wa imani. Hebu tusema kilikuwa na misingi minne. Msingi wa imani ulikuwa Ibrahimu. Msingi wa upendo ulikuwa Isaka. Msingi wa neema ulikuwa Yakobo (neema ya Mungu kwa Yakobo. Kila mtu anajua hilo). Bali katika Yusufu ulikuwa ukamilifu. Hapo ndipo Yeye angaliweka ile sanamu, juu ya, si ule msingi wa kwanza, msingi wa pili, msingi wa tatu, bali juu ya msingi wa nne.

63 Ibrahimu alimdhihirisha Kristo, bila shaka, vivyo hivyo Isaka naye katika upendo. Ibrahimu alifanya hivyo katika imani. Isaka katika upendo. Yakobo alifanya hivyo kwa neema yake, kwa sababu *Yakobo* maana yake ni "mdanganyifu"; na hivyo ndivyo alivyokuwa. Lakini neema ya Mungu ilikuwa pamoja naye. Bali kuhusu Yusufu, hakuna neno dhidi yake, ni alama moja ndogo tu, (kwa kuwa msingi hauna budi kuwa kipeo pia), alipomwambia baba yake, yule nabii, "Mwambie Farao ya kwamba watu wako ni—ni wafuga ng'ombe na siyo wachungaji, kwa sababu mchungaji ni chukizo kwa Wamisri."

64 Bali wakati huyo nabii mzee alifika mbele ya Farao, alisema, "Watumwa wako ni wachungaji." Kwa hiyo ikaikwaruza. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu ingali bado inakifanya kipeo.

65 Sasa, ule msingi uliwekwa kupitia imani, upendo, neema, na kwa ukamilifu kupitia kwa wale wazee wetu.

66 Sasa, kiwiliwili cha kipeo hiki kikuu kilikuwa manabii, ambao walikuwa Neno. (Natumaini mnaweza kuisoma. Mnaona?)—manabii, si torati, manabii. Kwa kuwa manabii walikuwa Neno lililothibitishwa ambalo linafanyika ule mwili, siyo wale wazee wetu, wale manabii. Wao walikuwa Neno.

67 Hatimaye, kwa kuwa Yeye alianza kule nyuma kabisa katika siku za Musa na akaja akawafikia manabii, kwa kila mmoja, hatimaye—akiujenga ule mwili, ukija karibu wakati wote . . . Na aliyekuwa mkuu wa wote alikuwa Yohana. Biblia ilisema hivyo. Yesu alisema hivyo: "Hakuna mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama Yohana Mbatizaji," kwa sababu alikuwa ndiye angelimjulisha Yule Neno. Kisha mwishowe kikaja kile Kichwa

kikuu, Kichwa cha wote. Mwili mwingine wote ulinena tu habari Zake.

68 Msingi uliwekwa na wazee wetu, bali kiwiliwili kikajengwa na Neno, ambalo lilikuwa manabii. Na hapa kinakuja Kichwa cha hao wote; Yesu akajitokeza. Hapo wakati hiki Kifuniko kiliwekwa juu yake, tunapata katika Yeye kazi yote ya mikono ya Mungu. Tunaona katika Yeye dhihirisho kamilifu la Neno, kwa kuwa alikuwa Neno, utimilifu wa Neno. Sasa tena Mungu ana Kipeo kikamilifu tena, kama alivyosema Isaya, "Tazama Mtumishi Wangu, Kipeo Changu ambacho nilikionyesha katika nyakati zote za huyu Mtu mkamilifu anayekuja. Na ndiye Huyu hapa amesimama mbele Zangu, mkamilifu. . ." Hapo katika mfano Wake akimdhihirisha Mungu. . . Kwa maana Yeye alisema katika Yohana Mt. 14, "Mnaponiona Mimi, mnamwona Baba."

69 Na halafu, "hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu;" naye Neno alichongwa akaonyesha jinsi Neno lilivyokuwa hapo mwanzo. Yeye, Neno, akidhihirishwa kwa kile Kipeo katika sura Yake, Mungu amerudi tena katika sura Yake, umbo la Neno likidhihirishwa katika mfano wa mwanadamu—kile Kipeo.

70 Manabii wote walikuwa na mawaa. Hao wote walikuwa ni sehemu. Bali hapa mwishowe anakuja yule Kipeo akipitia kwao, yule Mtu mkamilifu, hamna dosari kabisa ndani Yake, mkamilifu sana, akidhihirisha alivyo yule Mjenzi Mwenyewe. Sura Yake ilidhihirishwa katika Kazi Yake. Mungu na Kristo walikuwa Mmoja, hivi kwamba Yeye aliweka Roho Wake ndani Yake; na kisha hata ule mfano na yule Mjenzi wakawa Mmoja. Mungu na kazi Yake ya kuchonga, Kipeo Chake. . . Ambapo Musa—Musa aliyekuwa katika kazi ya San Angelo alikuwa—ama Michelangelo, hasa, ilikuwa ni—ni—kazi ya kuchonga sanamu iliyokuwa imekufa, kwa sababu ilikuwa imetengenezwa kwa jiwe. Bali hapa yule Mkuu wa Wajenzi, wakati Yeye alipoikamilisha Kazi ya Mikono Yake, aliingia ndani Yake.

71 Mkombozi wa mwanadamu aliyekuwa amekamilika, mkamilifu kabisa, mcha Mungu sana (hata hivyo hapakuwepo na uzuri hata tumtamani Yeye), wakati huyu Mwana wa Mungu Aliye Hai aliyezaliwa na bikira alipokuwa mkamilifu kabisa, na mnyenyekevu, na katika mfano wa Mungu, hata yule Bwana mkuu aliyekuwa amepitisha uhai Wake kwa manabii (Naye alikuwa utimilifu wa manabii wote). . . Yeye alikuwa mkamilifu sana, hata Mungu alipoona hivyo, Yeye akampiga Huyo na kumwambia kwa sauti kuu, "Nena!" kama alivyofanya Michelangelo, "Nena!"

72 Unasema, "Hiyo ni kweli?" Marko Mt. 9:7, tunaona juu ya Mlima wa Kugeuzwa, wakati ambapo alisimama Musa, torati, akasimama Eliya, manabii. Kutokea nyuma kabisa tangu wale wazee wetu, wale waanzilishi, torati, manabii, na hao

wote wakisimama pale, tunasikia Sauti ikishuka kutoka katika wingu ikisema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, msikieni Yeye!” Na kama watasikia, Yeye hana budi kunena. Ilikuwa siku chache tu kabla hajapigwa. “Huyu Ndiye Mwanangu, ambaye napendezwa kukaa ndani Yake. Nimemfinyanga Yeye. Imenichukua miaka elfu nne kumfikisha Huyu hatua hii. Na sasa Yeye yu mkamilifu sana hata sina budi kumpiga Yeye ili apate kunena. Msikieni Yeye. Yeye Ndiye amefanywa mkamilifu. Yeye—Yeye ndiye kile Kipeo.”

73 Kumbuka, alidhihirishwa nyakati zote kule nyuma katika Agano la Kale. Tunamwona Yeye akiwa ule Mwamba jangwani, ni ule Mwamba uliopigwa kule jangwani: “Mimi ndimi ule Mwamba uliokuweko jangwani.” Lakini hilo lilikuwa jiwe; halikuwa limefikia ukamilifu wake bado. Bali katika mfano Hilo lilifuata Kanisa kutoa Kwake kile ambacho Yeye angeweza kutoa, na kuwapa Uzima hao ambao Yeye angeweza kuwapa Uzima. Bali Yeye alikuwa ule Mwamba jangwani. Hakuwa amefanywa mwanadamu bado. Alikuwa tu katika mfano.

74 Musa alimwona Yeye akisimama katika mwamba huu. Alimwona Yeye akipita, naye akasema, “Ni mgongo wa mwanaume.” Unaona, yule Mchongaji alikuwa akimwonyesha Musa mfano usiodhihirika wa Kristo, jinsi kile Kipeo kikuu kitakavyoonekana wakati kitakapokamilishwa. Yeye alipitisha Hiyo. . . Aliingiza—ama—ama alimwonyesha Musa awali ono la sura ya kile Kipeo. Ilikuwa mgongo wa mwanadamu ilipopita jangwani.

75 Kumbuka, Angelo angeweza kupaza sauti tu na kuipiga ile sanamu na kusema, “Nena!” Lakini ilikuwa tofauti kabisa kwa Mungu, yule Mchongaji Mkuu. Wakati Yeye alipomfanya mtu katika mfano Wake, mkamilifu sana hata akamdhihirisha jinsi alivyo Yeye, Mungu akanena kwa sura ya mtu, akionyesha kile Yeye atakachofanya. Alinena kwa manabii walipokuwa katika mfano wao usiodhihirika wazi, Yeye alipokuwa akiendelea kufikia Kichwa. Lakini Yeye wakati alipofikia Kichwa, alikuwa sura kamili ya Mungu. Alikuwa akijidhihirisha Mwenyewe. Kisha akapigwa kwa ajili yetu. . . Sasa Yeye ndiye kile Kipeo kwetu, Kipawa cha Mungu, Yesu Kristo, Uzima wa Milele. Natumaini kamwe hatutasahau hilo.

76 Tunapoona siku zikiingia giza, tunapoona vivuli vikishuka. . . Ninapobashiri ni mizunguko michache tu ya jua na taifa hili limekwisha. Je mnajua, jana, tarehe nne Julai, ambapo Thomas Jefferson alitia sahihi Ilani ya Uhuru, yeye pamoja na ile halmashauri iliyokuwa pamoja naye, na ile Kengele ya Uhuru ikalia, nasi tukatangazwa kuwa taifa huru. . .? Kulingana na historia hapajakuwepo na demokrasia wakati wo wote iliyodumu zaidi ya miaka mia mbili. Na hiyo ilikuwa mwaka wa 1776, tarehe nne Julai. Na tumebakiza miaka kumi na

mmoja pekee. Litafaulu? La! Haliwezi! Miaka kumi na mmoja, na likifanya hivyo, litavunja historia yote.

77 Nasi tunaona hali ya wakati. Tunaona hali ya watu. Tunaona hali ya siasa. Tunaona hali ya ulimwengu. Haliwezi kusimama! Halina budi kuzama kama Titanic. Halina budi kuzama! Kwa maana kuna. . .Kutoa nafasi—taifa moja hutoa nafasi kwa lingine wakati linapoanguka. Na ufalme huu hauna budi kuanguka na kila ufalme mwingine kutoa nafasi kwa ule Ufalme ujao ambao hauwezi kuanguka. Kwa kuwa tunapokea Ufalme ambao hauwezi kutikisika kwa njia ya hii sura kamili ya Mungu, kile Kipeo.

78 Mungu, wakati alipomwangalia Huyo, Yeye alivuviwa sana, Yeye alikuwa. . .Kumwona Huyo katika sura Yake na kuona ule—ule mfano Wake. Yeye alivuviwa sana ya kwamba itakuwa Kipeo kikamilifu cha Mkombozi—Yesu aliye Mkombozi. Hivyo Mungu, ili apigwe Mwenyewe, kwa sababu ya kulipia adhabu Yake Mwenyewe, Mungu na Kristo wakawa Mmoja, kusudi Mungu aweze kupigwa katika mfano huo. Angeweza kutiwa kovu. . .Na hiyo ndiyo sababu Isaya alisema, "Tulimdhania ya kuwa Yeye amepigwa na kuteswa na Mungu. Bali Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu; Yeye alichubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake tumepona."

79 Sura kamilifu ya Mungu - mtu, Mungu *en morphe* alikuwa amegeuka kutoka kwa Wa Kimbinguni hata ono. Nalo hilo ono likawa ile Sura. Halafu hiyo Sura ikapigwa kusudi Yule wa Kimbinguni aweze kuonja hali ya mauti, kile Kipeo kikamilifu cha Mungu. Hangaliweza kufanya hivyo katika Musa. Hangaliweza kufanya hivyo katika manabii. Isaya aliyekatwa kwa misumeno hata akakatwa vipande-vipande. . . Asingaliweza kufanya hivyo katika manabii waliopigwa mawe. Yeye asingaliweza kufanya hivyo, kwa sababu Yeye asingeliihisi. Kulikuwa tu na sehemu Yake. Lakini katika hiki Kipeo kikamilifu Yeye alikuwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Yeye asingaliweza kumdhihirisha Musa pekee, Yeye angaliweza kudhihirisha utu Wake wote katika Mtu huyu na aonje mauti kwa ajili ya jamii yote ya binadamu. Kipeo kikamilifu cha Mungu, Mungu, alivuviwa sana kwa kukiona Hicho, hata Yeye akawa Mkombozi wa nyakati zote kuzungumza kwa niaba ya wale walio kule nyuma ambao walikuwepo hapo awali na waliopo sasa.

80 Ahadi zote zilitimizwa katika Yeye. Yeye alikuwa Ukamilifu wa ukamilifu. Mifano yote ilitimizwa katika Yeye: Mkombozi aliye jamaa yetu katika Ruthu na Boazi; Mpaji-Sheria wetu kutoka Mlima Sinai; Nabii wetu kutoka jangwani, Yeye aliposhuka kutoka mlimani, Yeye alipokuja kutoka jangwani—Yeye alipokuja kutoka Umilele akawa mtu, ile Sura kamilifu.

81 Mungu, katika nyakati zote, akikatakata kwa wale wazee wetu, na kutengeneza jukwaa Lake, na akawaleta kutoka mambo mbalimbali ambayo angeuweka huu msingi juu yake. Juu Yake akaanza kulijenga Neno Lake (hao manabii), na hatimaye akafikia kwenye yule Nabii mkamilifu, ule Msingi mkamilifu, ono kamilifu alilokuwa nalo Mungu.

82 Na sasa, kusudi hili linene (Yeye ni Neno)—na ili Neno lipate kunena hana budi kuingia katika ile sura. Halafu kusudi sura hii ipate kunena, haina budi kupigwa. Yeye anaingia ndani ya ile sura. Ndipo kusudi ipate kunena, yule Mkombozi mkamilifu . . . Mifano yote ya Agano la Kale ilitimizwa katika Yeye.

83 Kama nilivyosema siku nyingine, Yehova wa Agano la Kale ndiye Yesu wa lile Jipya. Ndiyo!

84 Ni kama wengi wenu wanaume, wanawake wa rika yangu, tulikuwa na viwanda vingi vya dobi wa Kichina. Wachina walipokuja mara ya kwanza, walitoka Pwani ya Magharibi wakielekea upande wa mashariki, wakija kutoka mkoa wa Mashariki, wakija huku. Na walipofanya hivyo, hao watu hawakuijua lugha yetu na mila zetu, bali walikuwa dobi wazuri. Nao hawakuweza kuandika risiti kusudi upate kurudishiwa nguo zako. Bali Mchina, alikuwa na kadi ndogo kadhaa zisizoandikwa cho chote. Basi unapokuja kuleta nguo zako, yeye angeitwaa hii kadi na kuirarua kwa njia fulani kisha anakupa kipande kimoja, naye akakiweka kile kipande kingine. Na sasa, ni nzuri zaidi ya yale tuliyo nayo siku hizi, kwa sababu unaporudi kudai kilicho chako, vipande hivyo viwili havina budi kuungana. Usingeweze kuigiza hata ufanye nini. Hakuna namna ya kufanya hivyo. Unaweza kunakili herufi, bali hauwezi ukaigiza huo mraruo. Sharti kiungane kabisa na kipande hicho kingine. Kwa hiyo, nguo zako chafu ulizozileta, ungeweza kuzikomboa kwa risiti hii, kwa sababu ililingana na risiti iliyoachwa.

85 Na wakati Mungu, kwa njia ya manabii chini ya torati, alipotuhukumia dhambi . . . Na torati haina neema; hiyo—inakwambia tu wewe ni mwenye dhambi. Bali Yesu alipojitokeza, Yeye alikuwa ule utimilifu. Yeye alikuwa ule—ule utimilifu wa kila kitu alichoahidi Mungu. Yeye alikuwa mfano ulio sawa na mkamilifu wa ile ahadi. Hivyo basi, ahadi zote za Agano la Kale zilitimizwa katika Yesu Kristo. Isingewezekana kutimizwa katika Musa. Isingewezekana kutimizwa katika ye yote wa wale wanabii, bali zilitimizwa katika kile Kipeo. Na alilingana na yote aliyosema itakuwa. Vivyo hivyo Kanisa halina budi kulingana na kila kitu ambacho Mungu ameahidi. Lazima liwe kile kipande ambacho kiliondolewa Kwake kwa kupigwa. Kwa hiyo kama ile ya asili ni Neno, basi wale waliotolewa Kwake watakuwa Neno, wapate kulingana na ubavu Wake.

86 Kwa hiyo, Mchina . . . Ungeweza kudai . . . Pale ambapo torati inakuhukumu na kusema ulikuwa mchafu, na ulikuwa na hatia, na ingeweza kukutia gerezani; bali Yeye alipokuja, Yeye alikuwa Kipande cha Kuambatanisha ambacho kingeweza kukutoa, na kukurudisha pia, kuwa risiti kamilifu— ule ukombozi ambao Mungu alikuwa ameahidi nyuma kule katika bustani ya Edeni: "Mzao wako utakiponda kichwa cha nyoka, bali kisigino Chake kitakiponda—kitakiponda kichwa chake."

87 Sasa, tunaona hiki Kipeo kilicho kikamilifu ambacho Mungu alikuwa amekimaliza. Sasa, tunaona ya kwamba Yeye alikuwa yote yaliyoahidiwa kuwapo. Yeye ni ahadi zote, unabii wote, kila kitu ambacho Mungu aliahidi juu ya: "Mzao wako atakiponda kichwa cha nyoka." Sasa, Yeye asingeweza kukiponda kwa torati. Yeye asingeweza kukiponda kwa manabii. Bali Yeye alifanya hivyo wakati yule Mzao wa mwanamke alipofanyika Kipeo, Kristo. Alikuwa lile Jiwe aliloliona Danieli limekatwa kutoka mlimani. Yeye ndiye Yule angeweza kulipiga. Yeye ndiye yule angeweza kukiponda, kukiponda kichwa cha nyoka.

88 Maisha Yake yalilingana sawasawa na maisha ya Musa. Maisha Yake yalilingana na Daudi. Hebu tuone kama alikuwa hivyo, kama Yeye ndiye kile Kipande cha Kuambatanisha.

89 Mtazame Daudi, mfalme aliyekataliwa na watu wake. Alikuwa . . . Siku moja alipokuwa . . . Mwanawe alimwinukia akamwasi. Naye akayatenganisha na kuyagawanya majeshi ya Israeli. Naye alikuwa . . . Daudi alifukuzwa—au akafukuzwa na watu wake mwenyewe kutoka kwenye kiti chake cha enzi. Naye alipokuwa njiani akitoka, kuna mtu aliyemchukia; naye anatembea kule, akimtemea Daudi mate. Mlinzi akauchomoa upanga wake, akasema, "Nitamwachia yule mbwa kichwa chake, aliyemtemea mate mfalme wangu!"

90 Daudi akasema, "Mwache, Mungu alimwambia afanye hivyo." Hamwoni? Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko, Yeye anasimama kama Kondoo mbele ya wanaomnyoa, kimya. Mnaona? Yeye alisema hivyo. Labda Daudi hakujua aliyokuwa anasema. Lakini yapata miaka mia tano, mia sita baadaye ama mingi zaidi, Mwana wa Daudi alikuwa anapitia barabara zile zile, na Yeye alitemewa mate. Lakini angalia yaliyotendeka wakati Daudi kutoka kwa—kutoka kwa . . . Alipokuwa mtoro, naye ametoka uhamishoni, wakati alipo—aliporudi, mtu huyo alimsihi akimtaka amani na msamaha. Hata na wale waliompiga Yeye watamwona siku moja atakaporudi.

91 Nasi tunaona basi katika Yusufu, ya kwamba Yusufu alizaliwa mwana wa kipekee, wa mwisho, upande wa juu kabisa wa ule msingi, ambapo kile kipeo kilipaswa kujengwa. Ilikuja kuanzia imani, ukaja upendo, na tena neema; ikafikia ukamilifu. Na ilikuwa vivyo hivyo kutoka kwenye ile miguu ya kule mwanzoni, ikaendelea mbele hata ukamilifu katika Kristo.

92 Angalia, jinsi ambavyo alidhihirishwa katika Yusufu, upande wa juu kabisa wa ule msingi, mtu aliye mkamilifu zaidi ya hao wote. Tunaona ya kwamba Yusufu alizaliwa kwa familia yake; naye kweli alizaliwa na yule mwanamke halali, ambaye alikuwa mke wa Yakobo. Na tazama pia, ya kwamba wakati alipozaliwa, baba yake alimpenda; na ndugu zake wakamchukia bila sababu. Kwa nini wao walimchukia? Kwa sababu yeye alikuwa Neno. Waona ule msingi wenyewe? Oneni jinsi kichwa cha ule msingi kilivyokuja. Sasa angalia kikija kichwa cha ule mwili. Sasa, angalia Kichwa cha Bibi-arusi kikija. Mnaona? Yeye alikuwa Neno. Nao walimchukia kwa sababu alikuwa mwonaji. Aliona mambo awali, na akawaambia. Yalitokea; hata kama yalikawia jinsi gani, yalitokea vivyo hivyo. Na kwa kuwa alikuwa wa kiroho alitengwa toka kwa ndugu zake. Walipaswa kumpenda. Lakini walimchukia, kwa kuwa yeye alikuwa nabii na alikuwa wa kiroho. Nao wakamchukia.

93 Tazama, yeye aliuzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha, akatupwa shimoni, akadhaniwa amekufa, lakini alitolewa shimoni. Na wakati wa yale majaribu yake gerezani, yule mnyweshaji na—na mwokaji. . . Tunajua ya kwamba yule mnyweshaji aliokolewa bali mwokaji alipotea. Na katika gereza la Kristo msalabani, mmoja aliokolewa na huyo mwingine akapotea—wezi wawili, watu wawili wadhalimu.

94 Nasi tunaona alitolewa gerezani mwake hata kwenye mkono wa kuume wa Farao, hata kwamba hakuna mtu angaliweza kuzungumzia Farao, bila kupitia kwa Yusufu. Na Yusufu alipoondoka kwenye kile kiti cha enzi cha Farao, tarumbeta ililia Misri nzima, sauti ikatolewa iliyosema, "Pigeni magoti, kila mtu, Yusufu yuaja!"

95 Ndivyo itakavyokuwa kwa Yesu. Jinsi Yeye alipendwa na Baba yake na kuchukiwa na hao ndugu wa kidhehebu bila sababu. Aliuzwa kwa vipande thalathini vya fedha (kama ilivyokuwa), kisha akatupwa shimoni akidhaniwa amekufa. Pale msalabani, mmoja alipotea na mwingine akaokoka. Naye akatolewa msalabani, naye ameketi mkono wa kuume wa Mungu katika Ukuu, yule Roho aliye mkuu, ambaye alikuwa amedhihirishwa katika Yeye. Na hakuna mtu anayeweza kuzungumza na Mungu, ila kwa njia ya Yesu Kristo. Waza hilo! Na wakati Yeye atakapoondoka kwenye kile Kiti cha Enzi, atakapoanza kuondoka, tarumbeta italia na kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri . . .

96 Kumbuka, alikuwa mwana wa ufanisi. Kila alichofanya kilifanikiwa, kama ilikuwa gerezani au po pote pale, ilikuwa mafanikio. Na Yeye je hajawaahidia watoto Wake kwamba Yeye atafanya kila kitu kitende kazi kwa manufaa yao, kama ni magonjwa, gerezani, mauti, huzuni, cho chote kile, ya kwamba kitafanya kazi kwa manufaa ya hao waliompenda Yeye. Yeye aliahidi hilo, na sharti liwe hivyo. Halina budi kuwepo.

Imenenwa kwetu kwa mifano katika Yeye. Yeye alikuwa ile Sura kamilifu ya Mungu.

97 Sasa, tunaona hapa ya kwamba Yeye atakapokuja tena... Kumbuka, Yusufu kwa ufunuo aliuokoa ulimwengu kwa unabii wake mkuu. Ulimwengu ungalikufa kama siyo kwa sababu ya Yusufu. Na ulimwengu ungalikuwa—ungalikuwa umekufa kama siyo kwa ajili ya Yesu: "Kwa maana jinsi hii, Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila amwaminiye asipotee." Mungu anahifadhi Maisha.

98 Tunaweza kuendelea zaidi na zaidi. Kwa sababu Yeye alikuwa sawa tu na Daudi. Alikuwa sawa na Musa. Alikuwa sawa na Eliya. Alikuwa sawa na Yusufu. Kila kitu ni mfano, kilichotabiriwa katika Agano la Kale, kililingana na huo. Ni nini? Ikionyesha Mkombozi mkamilifu ambapo tungetia nguo zote chafu zilizochakaa katika kiwanda cha dobi na kisha twende tukazidai tena. Zimefuliwa katika Damu ya Mwana-Kondoo. Tunaweza kudai yaliyo yetu. Na kila alichokifia, tunaweza kukidai. Kwa hiyo Yeye alikuwa Neno kamilifu akidhihirishwa kwa mifano.

99 Ilimpendeza Mungu, yule Mchongaji mkuu, kumpiga Yeye, na kufanya hivyo jinsi hii. Tunamwona katika Isaya hapa tunaposoma: "Sisi sote tulimdhania Yeye. Tuligeuza nyuso zetu tusimwone Yeye. Hana uzuri hata tumtamani Yeye (kila mtu akizungumza habari Zake, kumdhihaki Yeye. Mimi ninazungumza habari Zake sasa siku ya leo. Kila mtu anamdhihaki Yeye. Unaona?). Tulimdhania—tulimwona Yeye (*kudhania* maana yake ni "kuangalia"). Tulimdhania Yeye kuwa amepigwa na kuteswa na Mungu." Bali Yeye... Kwa sababu gani alifanya hivi? "Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubuliwa kwa maovu yetu."

100 Sasa, tungeweza kuendelea mbele zaidi na zaidi katika jambo hili, lakini naamini mumefahamu ninayomaanisha sasa—Mungu akitengeneza tena kipeo Chake.

101 Lakini tusisahau ya kwamba hapo mwanzo wakati Yeye alipompiga Adamu ubavuni, Yeye alitoa kitu fulani ubavuni mwake. Sasa, kule kupigwa kwa Kristo kulikuwa na sababu fulani, apate kutoa Kwake, mmoja atakayekuwa jamaa, Bibi-arusi, apate kujitwalia Bibi-arusi. Kwa hiyo wakati Kipeo Chake alipokamilishwa, ndipo ilimbidi Yeye kukipiga, atoe Kwake, si kipande kingine, si kiumbe kingine, bali kiumbe kile kile.

102 Ndugu yangu, usione hili kuwa baya, lakini waza kwa dakika moja. Kama Yeye alitoa Kwake, kile kiumbe cha asili, ili amtengenezee Bibi-arusi... Yeye hakuumba kiumbe kingine; Yeye alichukua sehemu ya ule uumbaji asili. Basi kama Yeye alikuwa Neno, Bibi-arusi anapaswa kuwa nini? Hana budi kuwa Neno la asili, Mungu Aliye Hai katika Neno.

103 Kimberley, Afrika ya Kusini. Wakati mmoja nilikuwa nikiziangalia almasi, jinsi zilivyokuwa zikichimbuliwa kutoka ardhini. Nami nikaziona zimewekwa mle kama. . . Naam, yule—yule kiongozi wa ule mtambo ama hilo shimo alikuwa mmoja wa wasimamizi wangu katika mstari wa maombi. Nami nikaona almasi zenye thamani ya makumi elfu ya dolla zimelundikana pamoja; lakini hazikumetameta hata chini ya nuru. Nami nikamwambia huyo kiongozi wa mashimo hayo, nikasema, "Mbona hazimetameti?"

104 Akasema, "Mheshimiwa, hazijakatwa bado. Lazima zikatwe. Kisha zinapokatwa, ndipo zinarudisha nuru." Haya basi.

105 Kipeo hakina budi kukatwa. Sasa tazama. Kwa nini kikatwe? Kipande chake huondolewa? La, la! Kipande kilichokatwa kinafanywa sindano ya santuri. Nayo sindano ya santuri inawekwa juu ya rekodi ambayo ni muziki usioonekana kwa ulimwengu; lakini hiyo sindano ndiyo inayoutoa, inatoa tafsiri ya kweli ya Neno.

106 Maisha Yake yalilingana na ya hao watu wote. Ilimpendeza Mungu kumpiga. Na sasa, kwa nini alimpiga? Kwa sababu ile ile iliyomfanya akampiga Adamu.

107 Sasa, tunamwona Yeye amepigwa na kupigwa na Mungu na kuteswa, Mwana-Kondoo mkamilifu aliyeuawa kwa ajili ya wenye dhambi, Kipeo kikamilifu.

108 Sasa, kwa karibu miaka elfu mbili Mungu amekuwa tena akijitengenezea Kipeo, kwa maana Yeye alimpiga Adamu apate kipande kutoka Kwake (sehemu Yake), ubavu mmoja kumtengenezea mke. Na sasa, kile Kipeo kikamilifu alichokipiga Yeye kule Kalivari, Yeye alitoa kipande kutoka Kwake. Ni Agano Jipya, hivyo tu. Yeye alitimiza Agano la Kale. Sasa, ni Agano Jipya, kipande kingine cha kutimizwa. Mnaona, Agano Jipya na la Kale ni mume na mke (mnaona?); na ilichukua lile Jipya—la Kale kuonyesha awali lile Jipya. Kristo akaja, kile Kipeo, kutimiza hilo. Sasa Bibi-arusi Wake atatimiza kila kitu kilicho katika Agano Jipya. Kipeo kingine kinatengenezwa.

109 Kama ilivyomchukua Yeye miaka elfu nne kutengeneza hiki Kipeo, sasa imemchukua Yeye karibu miaka elfu mbili kutengeneza Kipeo kingine, Bibi-arusi wa Kristo, Kipeo kingine. Katika kufanya hivyo, Yeye anakitengeneza kwa njia Yake isiyobadilika, namna ile ile Yeye alivyotengeneza kile Kipeo, Neno Lake. Hivyo ndivyo Yeye anavyojitengenezea vipeo Vyake. Kwa sababu Yeye anaweza tu kuwa Kipeo kikamilifu wakati inapokuwa Neno kamili. Uchafu wo wote, takataka, miingizo, vitavunjika; lakini mbingu na nchi zitapita, bali hilo Neno halitavunjika kamwe. Unakumbuka, katika kukata almasi, inakupasa kuwa na chombo kamili kufanya hivyo, haiwezi kufanywa na kipande cho chote kile. Nimeona tani za

hivyo visaga vikiivunja kwa kishindo na kuziondoa hizo tani kubwa, na kuipitisha hiyo almasi moja kwa moja. La, hakivunji hiyo almasi. Inapaswa kukatwa.

110 Sasa, Yeye anafanya jambo lile lile kwa njia Yake isiyobadilika. Tunaona katika Malaki 3, Yeye alisema, "Mimi ndiye Mungu, nami sibadiliki." Hawezi kubadili njia Yake.

111 Sasa, kama alivyoanza katika Ibrahimu. . .Baada ya kuanguka kwa kile kipeo cha kwanza, Yeye alianza katika Ibrahimu, juu ya msingi, kutengeneza kipeo kingine. Alianza siku ile ya Pentekoste kutengeneza Kipeo kingine—ile Mbegu Neno ya asili. Alianza katika Kanisa la kwanza. Ilikuwa nini? Mbegu Neno, Neno lililodhihirishwa, ahadi iliyotolewa, Yoeli alisema, "Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Wangu. Wana wenu na binti zenu watatabiri. Wazee wenu wataota ndoto; vijana wenu wataona maono." Yale Yeye angefanya katika siku za mwisho—mbili—miaka elfu mbili ya mwisho.

112 Tazama. Nayo ilianza kama ile ya asili. Kama Yesu alivyosema, "Neno la Mungu ni Mbegu iliyopandwa na mpanzi." Na Yeye alikuwa huyo Mpanzi. Ile Mbegu ilikuwa Neno. Na tazama. Mbegu yo yote inayokaa peke yake haitendi cho chote. Haina budi kuanguka ardhini kutoa mazao yake tena. Na hii Mbegu, hilo Kanisa kamilifu, lilianguka ardhini kule Nikea, Rumi, lilipofanyika madhehebu.

113 Sasa enyi wanahistoria, kumbukeni, nanyi mtakaosikiliza ukanda huu, chunguzeni hilo muone kama siyo kweli. Kanisa lilikufa pale Nikea, Rumi, wakati lilipochukua mafundisho ya masharti na kanuni za imani badala ya Neno la asili. Ilikuwa nini? Mungu alikuwa ameonyesha kwa Kanisa hilo la kwanza ya kwamba Yeye alikuwa Mungu. Alikuwa na Kanisa lililokamilishwa; bali Kanisa hilo, kama mbegu nyingine zote, halina budi kuanguka ardhini likafa. Sasa, lilianguka ardhini, likafa, na kuoza.

114 Mwajua, nilisoma kitabu kimoja hapa si muda mrefu uliopita. Mtu mmoja aliandika ki—kitabu kilichosema; *Mungu Aliye Kimya*. Huenda ikawa mmekisoma. Nasahau, na—nafikiri Brumback. . .La, sijui—sina uhakika ni nani aliyekiandika. Lakini. . .Siwezi kukumbuka. . .Kiko kwenye chumba changu cha kusomea: *Mungu Aliye Kimya*. Alisema, "Mungu, miaka elfu mbili ya Nyakati za Giza alikaa kimya, na hakusogeza mkono, na akawaangalia wafia imani waaminifu wakiingizwa kwenye matundu ya simba na kuchomwa moto na Warumi; mauaji ya kila namna; na wanawake kuvuliwa nguo zao, nywele zao ndefu zikiteketezwa kwa kutumia rami na kuchomwa moto." Kumbukeni, nywele fupi zilianzia kule Rumi. Na wanawake wa Wakristo walikuwa na nywele ndefu. Kwa hiyo wao—wao wakazichovya katika rami, na kuzichoma moto,

na kuwachoma—nao wakiwa uchi—na kuwafanya waliwe na simba. Na huyu mwandishi anaendelea kusema, "Yuko wapi Mungu huyo?" Lo, upofu wa mwanadamu wakati mwingine! Je, haujui ya kwamba hiyo Mbegu ilipaswa kufa! Yeye hakujaribu kuwakomboa hao. Walikwenda chini katika ushindi! Walikwenda chini huku wakitokwa na damu na kufa, wakitoa uhai wao. Kwa nini? Ilikuwa Mbegu, ilipaswa kuanguka ardhini, kama I Yohana 12 inavyotuambia: "Chembe ya ngano haina budi kuanguka ardhini na kufia humo, na si kufa tu, bali kuoza." Lakini hilo dhehebu halikujua ya kwamba Uhai huo ulikuwa ungali mle ndani.

115 Ingawa kanisa lenyewe pale kwenye Baraza la Nikea la siku kumi na tano za mabishano ya kisiasa ya umwagikaji wa damu, wakati hao waungwana walipoingia wakitaka kuwaingiza hawa watu wakuu mashuhuri kanisani...Nao manabii wakatoka kwenye hilo jangwa kule, wakila mboga na kuvaa ngozi za wanyama, manabii halisi, nao wakawatupa nje. Kwa nini? Hiyo Mbegu lazima ianguke ardhini. Sharti ife.

116 Ilikufa katika zile Nyakati za Giza chini ya taka nyeusi. Walidhani imeangamia kabisa. Mwajua, Yohana Mt. 12:24, Yesu alisema, "Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, hukaa hali iyo hiyo peke yake." Na Kanisa la kwanza lilikuwa uzao huo, yule Bibi-arusi, ile Mbegu, lile Neno lililodhihirishwa ambalo lilianguka ardhini kule Nikea, Rumi.

117 Sililizeni, enyi Kanisa katika mataifa yote mtakaosikia hili, uchafu wenu ndio huo; ni hayo madhehebu! Hapo ndipo Neno liliposulubishwa, nao wakayakubali mafundisho ya sharti. Na kwa miaka mamia kadhaa ya Nyakati za Giza zile nguvu na dhihirisho la Neno vilifichwa kwa ulimwengu. Ukatoliki pekee ndio uliotawala. Sote tunajua hayo, kwa kusoma historia. Ukatoliki tu ndio uliotawala.

118 Bali hu—huwezi kuificha mbegu iliyochipua. Haina budi kutokea. Kwa nini? Yule Mchongaji Mkuu anaishughulikia. Ataijenga tena. Kwa hiyo Yeye—ile Mbegu ilikwenda chini, lile Neno.

119 Tunapomwona Mt. Paulo, Petro, Yakobo, Yohana, hao wote walioliandika Neno, na ulimwengu walio—Neno waliloliandika likawa hai na kuishi. Nalo liliishi. Na tunapoona ya kwamba lilipoanza kuiva, Yohana akaanza kuandika zile nyaraka. Alitupwa katika Kisiwa cha Patimo baada ya kuchemshwa katika mafuta kwa masaa ishirini na manne. Lakini Neno halina budi kutokea. Lazima liandikwe. Hawangaliweza kumchemsha Roho Mtakatifu aliye ndani yake kwa mafuta hata atoke, hivyo yeye akatoka yu hai. Kazi yake haikuwa imekwisha. Yeye alikufa kifo cha kawaida.

120 Polycarp, aliyekuwa mwanafunzi wa Yohana, akaendeleza Neno. Na kutoka Polycarp akaja Ireneo. Naye Ireneo, yule mtu

mkuu wa Mungu aliyeamini Injili ile ile tunayoamini, "Neno ni kweli!" Kanisa, likijaribu kulisonga litoke nje.

121 Hatimaye ikafikia Nikea, Rumi. Na huko likaanguka ardhini (baada ya Mt. Martin), naye aliuawa. Mt. Martin aliamini jambo lile lile tunaloamini. Alisimamia jambo lile lile: ubatizo wa Roho Mtakatifu, ubatizo wa maji katika Jina la Yesu. Yeye alishikilia jambo lile lile tunaloshikilia, naye alikuwa nabii, na aliamini Neno lote la Mungu. Na mwishowe wao walisulubishwa, na kupondwa-pondwa ardhini, nao wakalala mle kwa mamia ya miaka mpaka ikaoza, hiyo mbegu ya nje. Miili ya kale ilioza. (Nimekuwa kule San Angelo katika yale mapango ya kuwazika hao watu na nikaona walikofia na mifupa yao ilivyovunjika na kila kitu.) Hatimaye walioza hata mifupa yao ikatoweka, bali ule Uhai ulikuwa bado upo.

122 Ile chembe ya ngano iliyoanguka ardhini pale—kwenye Baraza la Nikea ilianza kuchipuka tena katika Martin Luther, kama nafaka yo yote inayochipuka ama ngano. Baada ya zile mbegu kuoza, uhai ukatoka. Na ikaanza kuzaa katika Martin Luther. Jambo gani la kwanza alilofanya? Kukataa dhehebu la Ukatoliki, akalipinga kwamba lilikosea; kwa kuwa alisema, "Wenye haki wataishi kwa imani." Ilikuwa nini? Uhai mdogo na mnyonge uliotoa miche midogo. Hao walikuwa Waluteri. Hakika haifanani na mbegu iliyoingia ardhini, lakini Uhai unatoka sasa.

123 Kisha ukafikia ubua. Ndipo ilitokea nini? Katika siku za John Wesley, alifanyaje wakati alipoleta utakaso? Alikaa na Neno, nalo lilifanyaje? Waluteri tayari walikuwa wameungana na kuunda madhehebu; kwa hiyo wakati ulikuwa umewadia kwa jambo fulani kutendeka. Kile kipeo kinatengenezwa sasa. Alifanyaje? Alifanyaje? Alilipinga hilo kanisa la Kianglikana na akaja katika matengenezo kama kishada. Ni nini? Ile mbegu inatoa Uhai, inakua sasa.

124 Sasa, ubua haufanani na mbegu, wala kishada.

125 Sasa, enyi ndugu wa Kipentekoste katika mataifa yote, nawatakeni msikilize, ndugu yangu, kama huu ndio ujumbe wa mwisho nitakaohubiri. Huu ndio kipeo changu. Mmeona wakati ngano, chembe ya ngano inayoanguka ardhini, inapoanza kufanyika tena—chembe yake tena?

126 Tazama maumbile. Maumbile hasa ni Mungu, Mungu akitenda kazi katika maumbile ndipo mambo yanawezekana. Lakini kutoka uamsho wa Kipentekoste, kama wanavyodhania, ilikuwa Mbegu. . .Haikuwa hivyo. Sasa tazama! Lakini kitu fulani kilijitokeza kinafanana na ile Mbegu. Sasa, tazama alivyosema Yesu katika Mathayo Mt. 24:24, ya kwamba hizo roho mbili katika siku za mwisho zitafanana sana hata ingewapoteza walio wateule kama yamkini.

127 Sasa, huo ubua haufanani kamwe na mbegu; wala kishada hakifanani na mbegu. Lakini tazama sasa, si katika siku za Luther, bali katika siku ya mwisho.

128 Jambo la kwanza (kuna wakulima wa ngano wanaoketi hapa)—kitu cha kwanza kinachotoka katika chembe ya ngano, ungefikiri hasa ilikuwa mbegu yenyewe, lakini ni nini? Ni lile ganda. Hutengeneza kitu kidogo upande wa nje, kama, cha kushikilia ile mbegu. Hutengeneza ganda. Lakini hilo ganda silo mbegu kama vile ubua ama kishada kisivyokuwa; ni mchukuzi tu wa ule uhai, ile chembe ya ngano ya Yohana Mt. 12, (mnaona?), Yesu akinena.

129 Ile ngano, baada ya ubua, baada ya Wesley, hutoa ganda, ambalo linafanana sana na ile chembe kuliko cho chote kile. Ganda linafanana sana na chembe—linaendelea kufanana na chembe wakati wote, ile iliyoingia ardhini. Na ubua unapotokea, una uhai ndani yake, bali hakika huo si ile chembe. Kishada kinajitokeza, mbelewele, bado si chembe. Kisha ganda linajitokeza. Nalo lina umbo la ngano, kama chembe ya ngano kabisa; bali hata hivyo hilo si ngano. Lina umbo lile lile, kabisa.

130 Wapentekoste walijitokeza tu kama vile ambavyo ngano ingefanya. Kila mmoja anatoka kwa mwingine, anatoka kwa mwingine; lakini wao ni wachukuzi tu. Wanaunda madhehebu. Na hivyo ndivyo Wapentekoste walifanya, waliunda madhehebu. Nao Wapentekoste walifanyaje walipojitokeza kama ile chembe hasa? Walirudi nyuma moja kwa moja, kama katika Ufunuo 17, kwa moja la madhehebu dada zake. Hivyo ndivyo ilivyo hasa—hivyo ndivyo alivyosema Yesu.

131 Sasa angalia. Injili itatokea kupitia kwa Luther, kwa Wesley hata katika Pentekoste. Na katika siku za mwisho itawapoteza hata walio wateule kama yamkini—walio wateule! Lo, enyi ndugu wa Kipentekoste, hamwezi kuona?

132 Ngano inapoanza ni kama tu mbegu inapoanza kuumbika kama mbegu; lakini ni ganda. Waliunda madhehebu, wakafanya jambo lile lile hasa walilofanya huku chini katika Luther. Katika Ufunuo 17 inathibitisha jambo lile lile la makanisa.

133 Sasa, ile Mbegu ya nafaka ya asili ilianguka kule Nikea, kwa kuwa ilikuwa ndiyo madhehebu ya kwanza.

134 Tazama! Hapa Uhai uliokuwemo katika ubua, kishada, wote unaishia kwenye Mbegu. Ule Uhai uliotoka katika ile Mbegu asili, ulipitia katika hatua mbalimbali, hatua tatu mbalimbali, kisha ukageuka hata ukarudia hali yake ya awali. Haleluya! Lo, jamani! Mimi ndimi mtu mwenye furaha kupita wote ulimwenguni kwamba Mungu angeniruhusu kuona Hili!

135 Tazama jinsi kwa ukamilifu Neno na haya—maumbile hutenda kazi pamoja. Kama vile tu tunavyothibitisha ufufuo: Mapambazuko; kuchwa kwa jua na kupambazuka kwa jua tena; jani likitoka mtini kuingia chini ndani ya—utomvu kuingia

mzizini, na kurudi juu na—na jani linarudi pamoja na utomvu tena na kupukutika ardhini. Uhai wa huo mti hulinyonya ukalirudisha, yale madini ya chokaa na shura, na kulirudisha moja kwa moja katika jani lingine tena. Unaona? Maumbile yote, kila kitu hutenda kazi pamoja na—na Neno la Mungu. Na hali hii iko hapa kikamilifu katika Nyakati hizi za Kanisa. Hiyo ndiyo sababu Roho Mtakatifu alishuka na kuchora vitu hivyo na kutufafanulia kwa jinsi Yeye amefanya. Hiyo ni kweli hasa.

136 Tazama hapa. Ule Uhai uliokuwemo katika ganda, ubua, na katika kishada, katika ganda, wote unakusanyika katika ile Mbegu. Nao Uhai uliokuwemo katika ubua, ulikwenda—mmoja ulikwenda kutengeneza mwingine. Kuhesabiwa haki kulitengeneza njia ya Utakaso. Utakaso ulitengeneza njia ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulitengeneza njia kwa Roho Mtakatifu Mwenyewe kushuka moja kwa moja katika ukamilifu, kurudi kwa Neno tena kujidhihirisha Lenyewe.

137 Bali kilichofanyika madhehebu, hufa. Kama vile Uhai katika Luther ulitumiwa kwa kumtengeneza Wesley. Na—na kutoka kwa Wesley ulikwenda kwa Pentekoste. Na kutoka Pentekoste kutengeneza ile Mbegu asili. Ukaendelea hata . . . Pentekoste ilitoka kwa Wesley hata wakati huo. Sababu ya Pentekoste kutoka kwa Wesley, kwa kuwa haikuwa madhehebu—Pentekoste ilikuwa hivyo. Pentekoste iliondoka ikaunda madhehebu. Nayo ilifanyaje? Ikageuka kuwa ganda. Ilionekana kama kitu chenyewe. Na mtu ye yote . . .

138 Wangapi wameisha ona chembe—chembe ya ngano ikianza kukua? Kitu kidogo kinachotangulia ni nini? Ni kama ile chembe hasa, lakini ni ganda. Mnaona zile hatua tatu? Ubua, kishada ama mbelewele, kisha ganda. Halafu, kutoka katika ganda inakuja ile Mbegu asili. Si Mbegu, ilikuwa ni Uhai wa ile Mbegu uliokuwa ukikua kupitia haya kufikia ile Mbegu. Amina, amina! Mnaiona? Ni nini? Ufufuo. Kurudi kwa kile Kipeo tena, kama kile kilichoingia ndani.

139 Pentekoste ilitoka kwa Wesley, kwa sababu Wesley alikuwa madhehebu. Pentekoste ilipotoka haikuwa madhehebu kisha ikageuka ikawa hivyo. Ilipaswa kufanya hivyo kusudi ifanyize ganda. Lile Neno la Uzima la kweli lililokuwa juu yake lilikuwa likienda wakati huo kufanyiza ile Chembe asili kupitia hatua hizi: kupitia kwa ubua, kisha katika mbelewele; kutoka kwenye mbelewele hata kwenye ganda; na kutoka kwenye ganda ukafanyika Mbegu. La . . . Ubua, kishada, ganda!

140 Wakiishi, wao walitoa katika uamsho wao wa hapo mwanzo kitu cha kushikilia sehemu fulani ya Uhai wa ile Mbegu; lakini walipounda madhehebu, huo Uhai ukaondoka humo. Hilo linathibitishwa na historia yote. Hakuna madhehebu

yaliyowahi kufanya jambo baada ya kuunda madhehebu. Yalikuwa yamekufa. Hiyo ni kweli.

141 Angalia, Uhai unaendelea mbele sasa. Unasonga mbele.

142 Angalia. Yale wamefanya, hawa wote wamefanya, yamethibitishwa na historia jinsi hasa kanisa limekuja, lisipate kumfaa Yeye tena. Dhehebu limewekwa katika rafu. Hakuna katika historia nzima ya kanisa baada ya mojawapo kufanyika madhehebu, ila kwamba lilikufa. Na hayo madhehebu yakafa na hayakuinuka tena. Hamwezi kuona? Watu walio vipofu, yafungueni macho yenu! Maumbile na Neno vikiungana pamoja na kuthibitisha papa hapa ya kwamba hii ni Kweli, ya kwamba hii ndiyo Kweli. Uhai huo huondoka kwenye ubua kutengeneza kishada; kutoka kwenye kishada hutengeneza kapi; na kutoka kwenye ganda hurudia asili tena.

143 Tazama, hayatamfaa Yeye tena. Uhai huu uko dhahiri sana katika safari yake ndani ya chembe ya ngano kuliko ulivyo katika mti. Mungu aliwaita watu Wake kama mti. Mnaona? Uhai hushuka chini katika mti kisha ukarudi juu tena, unashuka na kupanda tena. Mnaona? Unashuka chini kisha unarudi tena. Bali katika chembe ya ngano unapanda juu kutoka ubua asili kupitia katika ubua, kishada, na ganda; na kile kitu ulichopitia hufa hata hauwezi kurudi kupitia mle tena. Ni nini? Haufai tena. Unasonga mbele hata kufikia ukamilifu wake. Amina! Je, hamuoni kwa nini Yeye hakutumia madhehebu? Hawezi kurudi mle tena. Yamekufa! Bali Uhai unapitia kutoka moja ukaingia lingine. Mnaona? Wao waliweka kanuni za imani na kuingiza. . . " Mtu ye yote atakayeongeza neno moja ama kuondoa neno moja . . . " Mnaona? Amefungiwa nje. Lazima iwe ni mbegu ya Uhai ikisonga mbele.

144 Natumia hili sasa katika mfano wa Bibi-arusi, kile Kipeo kinachokuja. Kama vile Kipeo kilivyoanguka, kuna Kipeo kinainuka. Kipeo kilianguka kule—kule Nikea, Rumi. Baada ya Nikea, Rumi, alipitia katika hatua fulani; lakini anarudi tena kwenye kile Kipeo, amekamilishwa, kwa maana Huyo ni sehemu ya Neno lililonenwa na Yeye. Yeye atakuwa na Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi. Halitafungamana kwa njia yo yote na shirika lo lote ama dhehebu (kitu hicho kilicholaaniwa). Limepitia katika mambo kama hayo, lakini halitakuwa humo kamwe.

145 Tazama. Ile mbegu inakua. Huo Uhai unakua, si kurudi nyuma. Hapatakuwepo na ufufuo zaidi baada ya huu. Uhai unajitokeza kufikia ukamilifu wake, ufufuo.

Tazama, ganda likitoa . . . Lile—lile . . . Tazama, kapi linatoa ile Mbegu asili kutoka ndani yake. Katika Ufunuo sura ya 3 tunaona hili.

146 Sasa kumbukeni, Yeye hakutolewa ndani ya kanisa lingine katika Biblia, kati ya zile Nyakati Saba za Kanisa. Wangapi

wanakumbuka hivyo? Yeye alipitia katika Wakati wa Kanisa kwenda kutengeneza kitu kingine. Lakini ndicho hiki. Hakuna kingine. Bali yule—yule Fundi-Mchongaji amerudi kwenye ukamilifu tena, lile Neno. Mnaona? Harudi nyuma. Ni tofauti jinsi gani. Ndiyo!

147 Lo, tena tazama. Wakati huo, ganda linapojitokeza huonekana tu kama Chembe. Lakini wakati Uhai wa hiyo Chembe unapoanza kuondoka kwenye kapi kuingia, kutengeneza ile Chembe (Bibi-arusi), kapi hufunguka na kuitenga Chembe. Je, hiyo ni kweli katika maumbile? Hivyo ndivyo lilivyofanya hasa.

148 Katika—katika Ufunuo 3 tunaona kwamba Wakati wa Kanisa la Laodikia ulimtoa Yeye nje. Sasa angalia, haikutendeka katika nyakati zile zingine, kwa sababu kulikuwa na kutengenezwa kwa kitu kingine bado. Ulipita tu na kwenda katika mwingine. Nimewaambia sikuzote, hakuna madhehebu mengine yanayokuja. Tuko mwishoni. Nao wakamtoa nje, kwa nini? Yeye—Yeye—Yeye ni Neno tena. Yeye ni kama lile lililoangukia kule. Yeye ni fundisho lile lile lililotoka tangu mwanzo.

149 Na wakati Mbegu Neno lnapoanza kukua, ganda linajiondoa kwake. Uhai unaacha mengine yote upate kulifuata; hao ni waamini wa kweli, wao hufuata huo Uhai, popote huo Uhai uendapo.

150 Kama katika Israeli, mfano kamili. (Kama tungalikuwa na wakati. . .Nina dakika chache tu zilizobakia.) Lakini katika huo mfano kamili hapo mwanzo, kila mahali ile Nguzo ya Moto ilikokwenda ulikuwa Uzima; Mungu alikuwa hiyo Nuru. Na sijali kama ilikuwa usiku wa manane ama kama wao walikuwa mahali pazuri palipochaguliwa, wakati hiyo Nguzo ya Moto iliposonga mbele, tarumbeta ilipigwa nao Israeli wakaondoka pamoja Nayo. Haleluya! Na wakati tarumbeta ilipopigwa, Martin Luther aliondoka pamoja Nayo. Naye akaunda madhehebu. . . Akafa. . . Si yeye binafsi, ni mtu yule aliyemfuata. Kisha Mungu akaondoa ule Uhai kutoka humo, akauleta Huo, akaulaza Huo katika kaburi.

151 Kisha akatokea Wesley. Aliona hayo madhehebu makubwa kwa hiyo akapiga tarumbeta ya utakaso, Neno zaidi. Mnaona? Na alipofanya hivyo, wao wakatoka, moja kwa moja kutoka kwa—kwa—moja kwa moja kutoka Luther wakaingia katika Methodisti.

152 Na wakati Pentekoste walipoiona, wao wakapiga ta—tarumbeta. Wakati umewadia wa kurudishwa kwa zile karama. Mnaona walilofanya? Walipiga tarumbeta, ndipo wakatoka; kisha wakaunda madhehebu. Lakini kumbuka. Baada ya kapi (hizo ndizo hatua tatu tunazojua) hakuna kilichosalia ila ile Chembe. Ee, Mungu! Na kisha ile Chembe hutengwa na yote

yale. Amina na amina! Mbegu, Neno linaanza kujiumba, na Uhai unatolewa kwake. . .

153 Angalia sasa. Kama Bwana Arusi, hapo mwanzo, yule Bwana Arusi wa kwanza. . .Huyu ni Bibi-arusi anakuja. Kumbukeni, Kanisa lilianzia kule Pentekoste, kisha likaanguka pale Nikea. Lilichipuka, si kama ile chembe halisi, la; ilikuwa sehemu ya Uhai mle ndani, lakini lilichipuka kusudi liunde madhehebu. Kisha likajitoa kwenye hayo madhehebu. Na kisha yakafanyaje? Basi yakaenda—kutoka kwenye hayo madhehebu kuingia kwenye madhehebu mengine, likaingia kwenye hatua nyingine ya Neno; Kuhesabiwa Haki, Kutakaswa, Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unaona? Na ulipokuwa unapitia kwenye huu ubua na hatua zingine, ulizidi kuongezeka.

154 Kumbuka, ile mbelewele ndogo ni zaidi—kishada kinafanana sana na Mbegu kuliko ubua ulivyo. Nalo ganda linafanana sana na ile Mbegu kuliko kishada kilivyokuwa. Lakini Mbegu yenyewe ni zaidi ya hicho. Mnaona? Ilikitumia hicho tu kwa usafiri katika kujisafirisha.

155 Angalia. Bibi-arusi. . .Kama Bibi-arusi hapo mwanzo alikuwa Neno—ama Bwana Arusi: kisha, iwapo Bibi-arusi ametolewa kutoka kwa Bwana Arusi, lazima Awe Neno pia.

156 Angalia. Bibi-arusi hana budi kuwa. . .Kwa nini? Kwa nini Bwana Arusi awe Neno lililodhihirishwa, lililowekwa wazi? Ni kwa sababu Bibi-arusi na Bwana Arusi ni Mmoja; Yeye ni kipande tu kilichokatwa kutoka Kwake. Huyo ndiye Kipeo. Alipigwa.

157 Michelangelo hangaliweza kuchonga hicho tena; hangaliweza kukirudisha tena. Bali Mungu atafanya hivyo. Atamleta tena Bibi-arusi huyu aliyekatwa katika ubavu wa lile Neno asili. Na ndiye Huyo hapo: huyo hapo yule Kipeo, ile jamaa imerudishwa tena katika bustani ya Edeni.

158 Huyu Bibi-arusi atafanya jambo hili vipi? Hii Ngano itafanya jambo hili vipi? Malaki 4 ilisema katika siku za mwisho itarudishwa. Nini? Kurudishwa kama ilivyokuwa hapo mwanzo, kuirudisha. "Nitawarudishia, asema Bwana, miaka yote iliyoliwa na tunutu, na parare, na yote yaliyoliwa na vitu hivi vingine. Nitawarudishia tena." Malaki 4 ilisema Yeye atairudisha mioyo ya watu, imani ya watu iwarudie wale baba wa hapo mwanzo tena. Unaona? Tunaona haya moja kwa moja mbele zetu, enyi Kanisa. Tuko wapi?

159 Sasa, tutafunga katika dakika chache. Nataka muangalie kwa makini sana jambo fulani lililotendeka.

160 Malaki 4 ni kurudisha, kurudi kwa asili. Amepigwa akatolewa katika kanisa—kutoka mwili wa kanisa, akapigwa pamoja na Bwana wake kwa kusudi lile lile (Yeye ni Neno), kama vile Yusufu alivyopigwa akatolewa kwa ndugu zake, kwa sababu alikuwa Neno. Na Yesu alipigwa akatolewa kwa ndugu

Zake, kwa sababu Yeye alikuwa Neno. Kanisa limepigwa—Bibi-arusi amepigwa akaondolewa katika kanisa, kwa sababu Yeye ni Neno. Ndizo hizo hatua zenu tena: moja, mbili, tatu. Mnaona? Vivyo hivyo hasa.

161 Neno, lililo hai na linalotenda kazi, Bibi-arusi wa Biblia, siyo Bibi-arusi aliyefanywa na mwanadamu, Bibi-arusi wa Biblia, aliyepigwa na kuteswa na Mungu. Hana uzuri hata tumtamani Huyo, hata hivyo tulimdhania, amepigwa na Mungu na kuteswa. Hiyo ni kweli. Yeye anasimama peke yake. Amepigwa na kutolewa katika madhehebu yote kulingana na Ufunuo 3. Amepigwa akaondolewa katika Wakati wa Kanisa la Laodikia alikolelewa. Unaona?

162 Kanisa hili lilikulia katika Wakati wa Kanisa la Laodikia. Hilo ni lile ganda. Lakini kama hao wengine walikwenda... Je, ninyi Wapentekoste hamwezi kuona hilo? Kama hilo lingine lilikuwa ganda na likafa, kama huo ubua mwingine ulipasa ufe, kama kishada kilipaswa kufa, vivyo hivyo hilo ganda lazima life. Zile hatua tatu za madhehebu.

163 Nanyi mnakumbuka... Mlisema, "Vema sasa, kuna vishada vingi sana vinavyoning'inia; kuna vitu vingi sana vya hivi." Naam! Wamekuwako Methodisti, Batisti, Presbeteri, Waluteri, Kanisa la Kristo, vitu hivi vingine vyote vilivyoliangukia, majani na kila kitu yalikuwa yananing'inia kwake; bali la asili lilikuwa yale matengenezo. Sasa, mnaona?

164 Anasimama peke yake, kama Bwana Arusi, amekataliwa na watu, amedharauliwa na kukataliwa na makanisa. Bibi-arusi yuko hivyo. Ni nini? Ni Kipeo Chake. Mnaona? Ni Neno Yeye analoweza kutendea kazi kwake na kulidhihirisha—likikataliwa.

165 Kwa hiyo ule ubua, kile kishada, na lile ganda havifanyiki Mbegu kamwe (la!), bali wakati wote vinaendelea kufanana zaidi na zaidi na ile Mbegu. Sasa, wakati wa mavuno ile Mbegu inarudia Uhai wake wa asili, inarudi kwenye Biblia. Malaki 4 ilisema kuwa ingaliletwa namna hiyo. Lo, lo, jamani!

166 Lazima iwe na lote... Kusudi ipate kuwa hivi lazima iwe na Neno lote. Hiyo ni kweli?

167 Sasa, Yeye alisema ni nini kingetokea katika Ufunuo 10? Safari ya Tucson ilikuwa na sababu gani? Kuweka wazi kwa Kanisa... Katika siku za mjumbe wa malaika wa saba (Ujumbe wa malaika wa saba) Neno lote la Mungu lingedhihirishwa. Muhuri wa yale yote yaliyoachwa na ubua, naam, na mambo yake yote, yangedhihirishwa katika wakati huu. Je hivyo ndivyo Neno lilivyosema? Ndipo tunaliona. Basi tuko wapi? Unaona? Tuko wapi? Kuna jambo moja tu. Mavuno yako hapa. Ameiva kabisa. Yuko tayari kwa kule kuja.

168 Tazama. La, halitakuwa hilo kamwe. Ule... Wakati wa mavuno Mbegu inarudi katika hali yake ya asili, na lazima iwe

na Neno lote kusudi ipate kuwa ile Mbegu. Na haiwezekani kuwa na nusu ya mbegu; haitakua. Lazima iwe ni Mbegu nzima. Siyo kwamba idhihirishwe, kusema, "Naamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Haleluya! Naamini katika kunena na lugha." Hiyo ni sehemu tu ya hiyo Mbegu. Lakini sasa, hiyo imeongezewa. Haleluya! Mnaona? Ule Uhai, si zile karama, ule Uhai wa hizo karama. Mnaona? Mnaona ninalomaanisha? Tuko katika wakati wa mwisho, ndugu zanguni.

169 Ubua, kishada, ganda vimekufa na kukauka sasa. Kuna jambo moja tu ambalo yapasa litendeke kwa vitu hivi, vitakusanywa katika Baraza la Umoja wa Makanisa Ulimwenguni vipate kuteketezwa kwa moto.

170 Neno limefanyika mwili, kwa jinsi hasa alivyoahidi katika Luka 17, na Malaki 4, na kila mahali. Mnaona? Hiyo ni Kweli. Funuo. . .

171 Uhai wote wa kweli uliokuwemo katika ubua, kishada, na ganda sasa unakusanyika katika ile Mbegu, tayari kwa ufunuo, tayari kwa mavuno. Alfa imekuwa Omega. Ya kwanza imekuwa ya mwisho; na ya mwisho ndiyo ya kwanza. Ile Mbegu iliyoingia ndani imepitia katika hatua fulani na imekuwa Mbegu tena. Ile mbegu iliyoanguka katika bustani ya Edeni kisha ikafa kule, ilirudi (kutoka kwa ile mbegu isiyo kamilifu iliyokufia kule)—ikarudi ikawa Mbegu kamilifu—Adamu wa Pili.

172 Hawa wa kwanza aliyeanguka, na akatumiwa katika yale matengenezo ya pili—kuja kwa pili, kwa kumzaa mtoto, sasa amekuwa Bibi-arusi wa kweli tena, ile Mbegu, kurudi moja kwa moja kwa Neno asili tena. Alfa na Omega ni sawa. Yeye alisema, "Mimi ni Alfa na Omega." Yeye hakusema kuhusu cho chote hapo katikati. "Mimi ni Alfa na Omega, wa Kwanza na wa Mwisho." Naam bwana!

173 Ile huduma ya kwanza na huduma ya mwisho ni sawa. Ule Ujumbe wa kwanza na wa pili—Ujumbe wa mwisho ni sawa. "Mimi ndimi—Mimi nilikuwa katika Alfa; Mimi niko katika Omega." "Kutakuwa na siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku, bali wakati wa jioni kutakuwako Nuru." Mnaona? Alfa na Omega; imekuwa ya kwanza na ya mwisho. Lo, jamani, ndugu zanguni, tungaliweza kukaa sa—masaa kadha katika jambo hilo.

174 Kipeo kikuu cha jamaa, yule Adamu wa Pili na Hawa wa Pili sasa wako tayari kwa ajili ya ile bustani, ule Utawala wa Miaka Elfu (Amina!) kurudi duniani. Haleluya! Yule Mchongaji Mkuu hakuwaacha wakae pale. Alichukua wakati kama Yeye alivyofanya katika mamilioni ya miaka akiwafinyanga mume na mke wa kwanza wakamilifu. Nao wakaanguka. Sasa imechukua miaka elfu kadhaa; Yeye amefinyanga tena; na sasa, wako hapa wakiwa tayari.

175 Yule Kipeo amekuja na kupigwa. Kutoka ubavuni Mwake amekuja msaidizi. Naye amepitishwa katika hatua zile zile.

Sasa, yuko hapa tena huku maumbile yote, Biblia, na kila kitu kinginecho, vikionyesha tumefika.

Mataifa yanavunjika; Israeli inaamka,
Ishara zilizotabiriwa na Biblia;
Siku za mataifa zimehesabiwa,
(Tazama huu upuuzi mtupu tulio nao!)
Zimekumbwa na hofu kuu,
Rudini, Enyi mliodharauliwa, makwenu. (Hiyo ni kweli. Yakupasa kuingia mle upesi iwapo unakwenda.)

Niko karibu kufunga katika muda wa dakika tano, kumi.

176 Angalia. Kile Kipeo kikuu cha jamaa. Mume na mke hawawezi kuwa jamaa kweli isipokuwa wawe mmoja. Yawapasa wawe hivyo. La, sivyo, hao si jamaa nzuri— mke akivuta upande mmoja na mume upande mwingine. Jambo hilo lingeifanya iwe jamaa mbaya sana. Bali katika mapatano, wakiwa na upendo mmoja kwa mwingine, hiyo ni familia. Na sasa, hiyo ndiyo ilikuwa kipeo cha Mungu; na jamaa zote za kweli hapa huonyesha hivyo. Mnaona? Na sasa ile familia iliyo kipeo imekuja tena—Kristo na Bibi-arusi Wake, wako tayari kuja. Yule Adamu wa Pili, Hawa wa Pili, wako tayari sasa kurudi nyumbani mwao. Na picha yote imekuwa ni ukombozi, kutoka mahali ilipokuwa, kuirudisha. Mnaona? Ndivyo ilivyo hasa. Kuirudisha tena.

177 Baada. . .Hivi majuzi nikisimama hapa kwenye Wafanyi Biashara Wakristo. . .Wengi wenu, nakisia, mlikuwapo. Nilipomsikia huyo kasisi wa Kiluteri (ama mhubiri, alidhaniwa kuwa hivyo) akisimama pale na kusema lile jambo la kipuuzi, na kufanya dhihaka kwa yale tunayoamini. . .Na hao Wafanyi Biashara wa Injili Yote wakimweka mtu huyo pale. Na kusema ya kwamba. . .Alivaa ukosi wake uliopinduliwa. Wengi wao hufanya hivyo sasa. Alisema, "Sasa, watu huniuliza kwa nini mimi huupindua ukosi wangu." Kasema. "Wanawezaje kukutofautisha na kasisi wa Kikatoliki." Akasema, "Hakuna tofauti, na haipaswi kuwepo." Akasema, "Sote tu watoto wa Mungu." Akasema, "Ninamjua kasisi wa Katoliki aliye kila mahali (mnaona?), anayeweza kuwa kila mahali."

178 Sasa, huwezi kuenea kila mahali pasipo kujua yote. Mungu hata haenei kila mahali; Mungu anajua yote. Kujua yote ambayo maana yake ni—humfanya Yeye aenea kila mahali (Yeye anajua mambo yote). Lakini kusudi awe kiumbe Yeye hana budi kuwa katika kiumbe kimoja. Bali akiwa mjua yote Yeye anaweza kuwa kila mahali, kwa maana Yeye anajua mambo yote. Aliyajua kabla ya. . .Yeye alijua kabla ulimwengu haujaanza ni viroboto wangapi, chawa, kunguni wangapi, na ni mara ngapi wangefumba na kufumbua macho yao, na kila kitu juu yake (mnaona?), kwa maana Yeye ameenea kila mahali. Nawe huwezi

kuwa mjua yote—mjua yote bila kuwa asiye na mwisho. Mnaona? Na kuna kitu kimoja tu kisicho na mwisho, Mungu. Amina!

179 Halafu sisi. . . Ni nini? Ni ibilisi, akiwapeleka moja kwa moja pale machinjioni, kila mmoja wao akiingia. Jinsi hasa Biblia ilivyosema. Na yapo hapa. Mnaona, yameingia moja kwa moja kati ya Wapentekoste na yakawavuta kabisa, kama tu. . . Ni wakati wa jinsi gani!

180 Lo, baada ya huo ushuhuda, mtu fulani aliniambia. . . Mimi—mimi. . . Ni jambo zuri kwamba sikusema mambo mengi sana, sababu wao labda wangalinipeleka kule gerezani; bali nilifikiria tu, "Hilo hapo." Wa—watu waliofundishwa, wanajua. "Wenye hekima watamjua Mungu wao siku hiyo," alinena katika Danieli. Naam, bwana! Mnaona? Wenye hekima watamjua Mungu wao; wao wanatazamia mambo haya.

181 Lakini ninapoona jambo hilo likitendeka, na hao Wapentekoste wakisimama pale pamoja naye. . . Hata Oral Roberts aliniangalia *hivi*. Nikasema, "Loo, jamani!" Umh!

182 Bali kusimama pale na elimu, na uungwana, wajua, na kadhalika. Hivyo sivyo Mungu anavyowaadibisha walio Wake. Yeye hawaadibishi walio Wake kwa elimu; Yeye huwaadibisha kwa unyenyekevu na katika nguvu za Neno Lake lililodhihirishwa, akionyesha umbo la ile Chembe walimotoka.

183 Sasa, mtu fulani aliniambia, akasema, "Ndugu Branham," akasema, "kuna jambo moja kwako nisiloelewa."

Nikasema, "Ni jambo gani hilo?"

Nikisimama kule nje ukumbini. . . Nakisia Dada Dauch na hao wengine, baada ya kupeana mkono na Bill, na nikisimama pale na hao wote, na nikazunguka pembeni na kundi nzima la watu, mhudumu akajipenyeza mle, ukosi uliopinduliwa, akasema, "Mbona wewe unawakemea watu kila wakati?" Akasema, "Watu hao wanaamini kuwa wewe ni mtumishi wa Mungu, uwe mpole na mzuri kwao na kila kitu." Kasema, "Kila ninapokusikia ukiinuka, unawakemea sana wanawake kwamba wana nywele fupi, na juu ya kuvaa kaptura, na kujipodoa, na mambo hayo mengine yote, na kuwakemea watu na kuwaambia jinsi walivyo baridi, watu wa kufuata desturi tu, na wasiojali." Kasema, "Kwa nini unafanya hivyo?" Kasema, "Watu hao wanakupenda. Wawezaje kuwa mwana wa Mungu anayewapenda watu na kufanya jambo kama hilo?"

184 Nikawaza, "Bwana, hebu nimjibu mtu huyu mwerevu. (Unaona?) Nijalie kumjibu kwa namna fulani ambayo itamfanya anyongwe na kamba yake mwenyewe. Ni—nikasema, "Vema. . . " Nikasema, "Mheshimiwa, je ulipata kusoma habari za yule mwanamuziki mashuhuri aliyeitwa—yule mtunzi mashuhuri jina lake Beethoven."

Akasema, "Naam, hakika, nilisoma habari za Beethoven."

185 Nikasema, "Huenda ikawa alirarua vikapu kadhaa vilivyojaa makaratasi yaliyotupwa, lakini aliukabidhi ulimwengu vipeo." Hakufungua kinywa chake na kusema neno jingine. Nikasema, "Alipokuwa ameketi katika chumba chake cha kusomea chini ya uvuvio, angeandika kitu fulani. Angeingia katika chumba chake cha kusomea na kuomba. Haukuwa sawa, angeirarua na kuitupa katika kikapu cha takataka. Bali alipopitia kwenye uvuvio wote, ulimwengu ukapata kipeo." Lo, jinsi Neno linavyokata, bali hutoa vipeo, huondoa makapi yote pamoja na ubua, ndipo linatoa Kipeo.

186 Nina dakika saba za kuwaambieni jambo lililotendeka juzi, tupate kuondoka katika wakati uliopangwa. Tarehe tatu Julai, nilikuwa humu nikikaa so—sokoni upande huu (madukani, upande ule kutoka hapa tulipo). Nimekuwa Pig Alley kule Rumi—kule Ufaransa, na nimekuwa katika Jiji la New York, Los Angeles; lakini kundi chafu sana la wanawake nililopata kuona maishani mwangu ni Jeffersonville, Indiana. Sijapata kuona upotovu mwingi hivi pamoja na uchafu maishani mwangu kama ninavyouona katika hao watu. Nilikaa pale hata moyo wangu ukauma, na Bwana alikuwa amenipa ono. Sasa, nitawaambia hilo ono. Sijui kama naweza kulifasiri, lakini ni—nitasimulia hilo ono kwa mara yangu ya kwanza.

187 Nilipatwa na njozi. Na iliponitokea hivyo, tulikuwa na mtu fulani. Sikumuona huyo mtu. Ilikuwa ni Sauti tu. Nami ni—nikaangalia. Na ni—nilipoangalia upande huu, Akasema, "Bibi-arusi atajitokeza apate kuonekana kimbele apate kukaguliwa." Kisha nikatazama wakija kwangu, nami nikaona kundi la wanawake walio—walio wazuri mno waliovalia mavazi nadhifu sana niliopata kuwaona maishani mwangu. Lakini kila mmoja wao, ilivyoonekana, alikuwa amevalia tofauti. Wote walikuwa na nywele ndefu, nao walikuwa. . . nguo zenye mikono mirefu na marinda marefu na kadhalika, wanawake vijana. Walionekana kama, ningesema kama, labda, wenye umri wa miaka ishirini.

188 Sasa, ninayo Biblia iliyofunguliwa mbele yangu. Mnaona? Naweza kusema tu yale niliyoona. Ukisema, "Unaangalia nini?" Ninaangalia saa. "Unatafuta nini?" Ninawatafuta watu—nikiwaangalia watu. "Unaangalia nini?" Ninaangalia Biblia. Hivyo ndivyo. . . Ninasema Kweli; hayo ndiyo ninayoona. Nami naweza kusema tu niliyoona. Si—sijui ni nini—maana yake, inanibidi tu kuwaambia.

189 Lakini wakati huyu Bibi-arusi. . . Alikuwa akiangalia moja kwa moja kwa. . . (Yule aliyekuwa akizungumza nami, nami—tukisimama pamoja.) Macho yake. . . Walikuwa watu walio wasafi sana na wazuri sana niliopata kuwaona maishani mwangu. Ilionekana kama wangeweza kufika dazani moja ama wengi zaidi, ni. . . Sijui wangapi waliokuwa sambamba, bali walikuwa kundi. Na Yeye akapita, kwa madaha, macho yake yameinuliwa, akienda kwa uangalifu alipokuwa akipita. Lo,

alikuwa mzuri Huyo! Nikamwangalia. Naye alipokuwa akipita, Akasema, "Sasa, tutakagua. . ." Kasema, "Huyo ndiye Bibi-arusi. Sasa, tutayakagua makanisa." Nayo yakaja. Nikayaona yakija. Ndipo yalipokuja, kila moja, lilivyoonekana, lilikuwa baya zaidi. Sijawahi kuona kundi chafu namna hiyo maishani mwangu. Naye aliposema, "La pili. . ." Nikasikia kelele. Nayo ikasema, "La pili," ikasema, "hapa linakuja kundi la Amerika."

190 Naam, mimi ni Mwamerika, lakini hili lilinifanya nichefuke moyoni. Mimi sina ufasaha wa maneno wa kutosha, katika wasikizi waliochanganyikana, kusema yale yaliyokuwa yakitendeka; mimi—mimi—mimi. . .Itakupasa kusoma katikati ya mistari. Lakini hao wanawake walipokuwa wanakuja, kiongozi wao alikuwa mchawi. Alikuwa na pua ndefu sana na mdomo mkubwa mno. Na hao wote walikuwa wamevalia kitu kama nguo za sehemu ya chini huku, bali upande wa juu ulikuwa na ukanda tu ambao—mdogo, ukanda kama wa nusu inchi uliofungiwa juu na ukawazunguka hivi. Na kila mwanamke alikuwa na kitu cha namna. . .Wengi wenu, miaka kadha wa kadha iliyopita mlikuwa. . .Mnakumbuka, wakati tulipokuwa tunakata hiyo karatasi, mnajua, gazeti, kutengeneza fungu la matamvua ya kale?

191 Wangapi wanakumbuka? Mnajua. Naam, nafikiri mliitumia katika sikukuu, mwajua. Vikining'inia hivyo, karatasi yenye matamvua, karatasi ya nyuzinyuzi. Walikuwa na kitu kimeshikilia sehemu zao za chini hivi, kimeshikilia upande wa chini. Sehemu hii yote ilikuwa uchi. Na kila mmoja wao alikuwa amekatwa nywele zikawa fupi sana, zimesokotwa kote, nywele zilizokatwa zikawa fupi sana, nao wamejipodoa kwelikweli. Hapana shaka ila walionekana kama makahaba wa mitaani. Nao walikuwa wakitembea na hii karatasi. Na utovu wa adabu! Sasa, karatasi ndiyo ilishikiliwa mbele zao: bali walipopitia jukwaa la kukagulia, nyuma yao. . .Na kuona jinsi walivyokuwa wakitembea kwa sehemu zao za mbele na za nyuma, na jinsi walivyokuwa wakitenda. . .Nikasema, "Je hilo ndilo Kanisa?"

192 Nalo likaondoka. Nao walikuwa wakiimba nyimbo hizi za twisti na rumba, mwajua, ama cho chote mnachoziita, huku wakiteremka. . .kama wanaoimba, wakienda nyuma. . . Nikasema, "Je hilo ndilo Kanisa?" Nami nilikuwa nimesimama pale. Moyoni mwangu nilikuwa nikilia. Naye huyu mchawi. . . Kwa maoni yangu si kitu kingine duniani, bali yeye ni—yeye ni Baraza la Makanisa Ulimwenguni likiwaongoza moja kwa moja barabarani kuelekea kule lilikokuwa likienda. Walikwenda wakatoweka mkono wa kushoto na wakatokomea katika machafuko matupu, huku wangali wakicheza muziki huu na kutoa sauti za kuchekesha sana, na wakiitikisa miili yao upande mmoja kisha upande mwingine, na kisha mambo mengine kama hayo, wakifanya yasiyofaa hivyo, wakitembea.

193 Nami nikaanza tu kukiinamisha kichwa changu, naye akasema, "Ngoja, Bibi-arusi lazima aje tena." Nami nikaangalia, nao hapa wanakuja tena. Nao wakapita, wanawake wadogo warembo. Wote walikuwa wakiniangalia moja kwa moja walipokuwa wanapita. Nikaona kwamba kila mmoja alivalia mavazi namna tofauti. Na yule aliyekuwa nyuma alikuwa na nywele ndefu zilizoning'inia chini nazo zimesokotwa hivi, huenda alikuwa Mjerumani ama mtu mwingine wa namna hiyo. . .Nami nikawaangalia. Kisha, walipoanza kuondoka, wawili ama watatu wao huko nyuma basi wakaacha kwenda kwa utaratibu. Nami nilikuwa niwakemee, nao wakawa wanajaribu kupiga hatua kwa utaratibu tena. Nami niliwaona tu—lile ono likatoweka na kubadilika kutoka kwangu.

194 Sasa, tafsiri yake ndiyo hii: Sababu. . .Sasa kumbukeni. Nilikuwa nimemaliza tu kuandika. . .Sikuwa nimemaliza, nilikuwa sijaandika hii mihitasari bado. Bali katika kuhubiri asubuhi ya leo, nilipata tafsiri yake katika mahubiri yangu. Je, mliona, kanisa lilionekana tu. . .Sasa, hiyo ni Kweli, marafiki. Baba wa Mbinguni, anayeliandika Neno, anajua ya kwamba ninasema Kweli. Mnaona? Najua—nasema tu Ukweli. Na bila kujua hilo jambo hadi dakika chache zilizopita, ilionekana kama au hivi karibuni. . .Unaona? Je uiona kwamba Bibi-arusi alionekana mara mbili? Ile Mbegu ya kwanza na Mbegu ya pili, zote mbili ni kitu kile kile hasa. Na sababu ya kuvalia—kuvaa mavazi ya namna mbalimbali, yeye atatoka katika mataifa yote, kumkamilisha Bibi-arusi. Kila mmoja wao alikuwa na nywele ndefu na bila kujipodoa, nao ni wasichana wazuri sana. Nao walikuwa wakinitazama. Hao waliwakilisha Bibi-arusi akitoka katika mataifa yote. Mnaona? Yeye. . .Kila mmoja wao aliwakilisha taifa moja, walipokuwa wakipiga hatua kikamilifu kulingana na Neno. Mnaona?

195 Halafu, yanipasa kumwangalia. Atakosa kupiga hatua kwa utaratibu wa hilo Neno nisipomwangalia, wakati anapopita, kama atanikaribia. Labda itakuwa wakati wakati wangu utakapokwisha (mnaona?), nitakapomaliza mwendo, ama cho chote kile.

196 Tazama! Wao walikuwa wakirudi, wakijitahidi wawezavyo. Walikuwa wanarudi: walikuwa wakiingia mstarini, maana walikuwa—walikuwa wakiangalia mahali pengine, wakiliangalia hilo kanisa lililoingia katika machafuko matupu. Lakini wawili. . .Hao waliokuwa mbele hawakufanya hivyo kamwe. Wale waliokuwa huko nyuma—wawili tu ama watatu wao, walitoka nje kidogo upande wa kulia, na ilionekana kama kwamba walikuwa wakijaribu kurudi mstarini walipokuwa wanapita. Walikuwa wakinipita, loo, kwa umbali wa kutoka hapa mpaka ukutani, wakinipita. Nami nilikuwa nimesimama pale. Kisha nikawaona wote wakitoka nje na kuondoka.

Lakini mnaona, kanisa lilionekana tu mara moja, kila taifa, kanisa. Bali Bibi-arusi alikuja mara mbili. Mnaona? Mnaona ilikuwa nini? Sasa, bila kujua jambo hilo, lakini liangalieni kwa ujumbe wangu asubuhi ya leo. Bila kujua jambo hilo. Mnaona?

197 Mbegu ilianguka ardhini kule Nikea. Hiyo ilikuwa ile Mbegu asili. Naye amepitia katika hatua za haya madhehebu ambayo yanaishi tu mara moja. Bali Bibi-arusi anarudi tena katika siku za mwisho: "Nami nitawarudishia." Mnaona? Kile Kipeo kinaletwa. Hiyo ndiyo sababu Bibi-arusi alionekana—alikaguliwa mara ya pili. Alikaguliwa mara ya kwanza, kisha akakaguliwa mara ya pili. Naye anafanana kabisa mara ya pili na Yeye alivyokuwa mara ya kwanza. Ee Mungu, turehemu! Hima, hima, hima! Uzima, ingieni katika ile Chembe upesi sana! Mnaona?

198 Hao wengine wote hawakuonekana tena. Waliondoka wasirudi tena. Bali Bibi-arusi alirudi, kwa sababu Yeye ni Alfa na Omega. Mungu, yule Mchongaji Mkuu, amejitengenezea Mwenyewe Kipeo, kwa maana Hicho ni kipande cha kile Kipeo Chake cha kwanza. Kama Yeye alivyotengeneza katika bustani ya Edeni na akatoa kipande kimoja kwake kisha akatengeneza kipande kingine, na hicho kiliharibiwa kikaanguka; sasa Yeye wakati huu wote amekuwa akikijenga tena. Na Yeye akatoa hiki Kipeo, nacho kikapigwa kusudi—hiyo sehemu iliyopigwa ilikuwa kusudi ilirudishe tena kile Kipeo tena.

199 Kwa hiyo kile Kipeo na Mwana wa Mungu—Kipeo na Bibi-arusi. . . Naye ni sehemu Yake, ambayo ni lazima iwe kutimizwa kwa Neno. Neno limekwishatimizwa, nasi tuko tayari kwa kule Kuja kwa Bwana.

200 Loo, enyi Kanisa la Mungu Aliye Hai, inamisheni mioyo yenu na— ninyi wenyewe mbele za Mungu! Mambo haya ni kweli. Najua ya kwamba ina—inasikika kana kwamba kitu kikuu kama hicho kingekuwa, kingesambazwa kote katika mataifa; haikuwa hivyo kamwe. Yeye habadilishi njia Yake.

201 Iweni na shukrani tu, Kanisa, iweni na shukrani ya kwamba mko mahali mlipo leo iwapo mko katika Kristo. Kwa sababu mnaona. . . Sasa. . . Na wakati hiyo. . . Kumbukeni, Uhai huo wote utakusanywa katika Chembe kwa ajili ya ufufuo, bali ubua hauna budi kuchomwa moto, na mengineyo. Ganda na mengine yote lazima kuangamizwa, na yataangamizwa. Msitumainie yaliyo yenu—hayo madhehebu. Dumuni katika Neno, ule Uzima, Mungu na Kipeo Chake.

202 Halafu, mna nini kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu? Kristo na Bibi-arusi, wamerudi katika bustani ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Amina!

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na akanunua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

203 Hapo ndipo Yeye alipopigiwa. Tulimdhania ya kwamba amepigwa, amepigwa na Mungu na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu.

204 Je kuna ye yote hapa asubuhi ya leo ambaye hayumo katika hiyo Chembe asubuhi ya leo? Na kama ilivyo kwamba Uhai sasa unavuta sehemu yake ya mwisho kutoka kwenye ganda, kwa kuwa ganda linakauka . . . Ni wangapi wanaojua ya kwamba kanisa la Kipentekoste linakauka? Ni kwa nini? Uhai unaliacha. Kwa kweli, tayari umeondoka kwake. Na iwapo huyo Bibi-arusi tayari ameonekana kimbele, nashangaa basi kama Bibi-arusi tayari hajafanyizwa.

> Nampenda, nampenda,
> Kwani alinipenda kwanza,
> Na akanunua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

205 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa. Je, kuna wengine humu ambao wangetaka kukumbukwa? Kama ukijisikia ya kwamba wewe si . . . Marafiki, ni dhahiri sana. Sijapata kuona ono maishani mwangu, pasipo jambo fulani kutendeka, likafuata. Ninawaambieni Ukweli. Nyakati hizi zingine zote iwapo nimewaambieni Ukweli, Mungu ameuthibitisha, basi ninanena Ukweli wakati huu.

206 Sijui tunaishi katika siku gani, bali najua hamna kilichosalia. Hakuna mwanasiasa angaliinuka na kusawazisha kitu hiki. Siasa, taifa hili limekwisha. Ee, Mungu! Mwaweza ku—kuingia kilindini kina cha kutosha ku—ku—kuhisi jambo hilo. Taifa hili limekwisha—si taifa, bali mataifa. Hili ndilo zuri sana la hayo, nalo limekwisha. Ndipo iwapo mataifa yamekwisha, ulimwengu umekwisha. Na makanisa je? Kwa maoni yangu, Pentekoste lilikuwa ndilo zuri sana walilokuwa nalo; lakini limekwisha. Ee Mungu, uturehemu sisi!

207 Iwapo humjui Yeye, tafadhali fanya hima, harakisha! Kama ukihisi ule Uzima, ondoka katika—ondoka katika dhambi yako, ondoka kwenye kitu ulichomo, ingia kwenye ile Chembe haraka. Utakufa katika ubua ama katika ganda. Omba, tunapoimba sasa.

> Nampenda, (Ni juu yako sasa. Hatuna madhehebu, hatuna kitu; tuna Kristo pekee. Unakaribishwa kuabudu pamoja na Yeye—pamoja nasi hata Yeye atakaporudi. Hatuwezi kuandika jina lako katika kitabu; hatuna vitabu. Tunataka jina lako liwe katika Kitabu cha Uzima. Unaweza kufanya hivyo tu kwa kuzaliwa. Mbona usifanye hivyo sasa hivi? Mwombe Kristo akupe Uzima mpya, akuingize ndani, uandikwe jina lako katika Kitabu Chake kama haliko

humo. Kisha unaweza kuabudu pamoja nasi.
Tungependa kuwa pamoja nawe.)
Nampenda . . .

208 Mungu Mpendwa, msaidie kila mtu sasa afanye uchunguzi, aone kama sisi tu ndani Yake. Wewe ulitupenda. Ulipigwa kwa ajili yetu. Nasi tulikudhania kwamba Wewe umepigwa na Mungu na kuteswa. Naomba, Mungu, ya kwamba utamwita kila mmoja. Bwana, zungumza na watoto wangu, niwapendao, na rafiki zangu. Tujalie, Bwana, sasa hivi, katika Jina Lake Yesu Kristo.

209 Usiache mtu ye yote angoje kwa muda mrefu sana, Bwana. Inaonekana imekaribia sana. Mavuno kweli yameiva. Chombo cha Mungu cha kuvuna kitapitia nchini mbio katika mojawapo ya siku hizi; majani makavu yatarushwa kila upande; bali Ngano itakusanywa ghalani, itwaliwe, kwa sababu katika Hiyo kuna Uzima. Tujalie, Bwana, kila ombi lijibiwe, kila sala idhihirishwe mbele Zako.

210 Nawaombea, Bwana. Naomba kwamba Wewe hutamwacha ye yote aliye hapa apotee, Bwana. Wali—wali—waliketi kwa shida. . . Wao—wao—wao husafiri kwa motokaa maili mia kadhaa. Na cho chote tunachohitaji, tupe, Bwana, cho chote kizuri kwetu, Bwana. Si kilicho chema machoni petu, bali kilicho chema machoni Pako. Tunataka kusimama kama bikira aliye msafi ambaye amerudiwa, amekemewa na Mungu, tupate kutakaswa dhambi zetu.

211 Nami nawaombea hao, Bwana. Si—si—sijui namna ya kuomba. Tuna—tunazungumza na Mwenyezi Mungu, na ni mwanadamu yupi aliyepo, ni binadamu gani awezaye kufanya ombi linalofaa mbele za Mungu Aliye Hai? Lakini, Bwana, maneno yangu yasiyotamkwa vizuri na—na majina yangu ya vitu na vijina ka—katika mahali pasipofaa, kama Wewe ungaliweza kutambua a-b-c za mvulana mdogo siku moja na kutunga sentensi, Wewe—Wewe waweza kuacha majina yangu ya vitu na vijina na uangalie tu yale ninayoamini, Bwana. Ninakuamini Wewe. Ninaamini hili Neno. Nami ninaamini kwa ajili ya kila mmoja hapa. Nami ni—ninawaleta kwenye hayo madhabahu, Bwana, kwa imani, mahali ambapo kati yetu na Yehova Aliye Mkuu pana Damu ya Mwana Wake, Yesu. Nayo hiyo Damu itanena kwa niaba yetu. Ulipompiga Yeye kule Kalvari, Wewe ulisema, "Nena! Msikieni Yeye!" Na hiyo Damu, Biblia ilisema, inanena mambo makuu kuliko damu ya mwana-kondoo katika Agano la Kale; kwa kuwa Damu ya Kristo inanena makuu kuliko damu ya Habili, mambo makuu zaidi. Nawe nena, Bwana, ukombozi kwa ajili yetu, tunapokuita kupitia ile Damu.

212 Baba Mkuu wa Uzima, tuingize ndani, Bwana. Kama—kama tumetenda dhambi, iondoe kwetu. Ha—hatutaki kuwa hivyo, Bwana. Si kusudi letu. Nasi tunatambua ya kwamba tunaishi

katika njia yenye giza la kutisha. Kama tulivyosema hapo mwanzo, tunapanda mlimani, kupitia sehemu zilizoparuzika; mkondo wenye utusitusi; bali tunabeba Taa. Jalia tuione Njia hatua kwa hatua tunapotembea sasa, hata tutakapokutana, kama *Safari ya Msafiri,* hata mwishowe tutakapofika juu ya kile kilima. Tuongoze, Ee Mchungaji. Yehova Mkuu, tuongoze kwa Roho Wako.

213 Nasi tunajua ya kwamba tuko mbali na kipeo, lakini tunaangalia tulikotolewa, kile Kipeo halisi, nasi tunamtumainia Yeye. Tupeleke tu Kwake, Bwana. Tujalie, Bwana.

214 Waponye watu wote walio wagonjwa hapa, Bwana. Tulimdhania ya kwamba Yeye amepigwa na kuteswa. Bali Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu. Kipeo cha Mungu kilipigwa. Na Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa. Waponye wagonjwa, Bwana, katika uwepo Wako wa Uungu sasa, tunapojua ya kwamba Wewe uko hapa.

215 Zitakase nafsi zetu, mioyo yetu kutokana na uovu wote, mawazo mabaya yote, mazungumzo mabaya yote, mambo yote mabaya. Tutakase. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utayaponya magonjwa yetu, na tujalie tuondoke hapa tukijisikia ya kwamba sisi ni watoto Wako waliotakaswa. Na huku Damu ikiwa juu yetu, tunanena kupita katika Damu, Neno. Tujalie, Bwana. Tunaomba katika Jina Lake Yesu Kristo. Amina.

216 Baba Mungu, juu ya hizi leso, zitie mafuta kwa Uwepo Wako, Bwana. Na Uwepo Wako uwe pamoja nazo ko kote ziendako. Po pote zitakapowekwa, juu ya mwili wo wote mgonjwa, jalia waponywe. Na cho chote kile, kama kuna nyumba iliyovunjika mahali fulani, itengeneze, Bwana, ewe Mchongaji Mkuu. Tujalie, Bwana.

217 Tufinyange na utufanye wana na binti za Mungu. Tunaamini ya kwamba Bibi-arusi anafanyiwa matayarisho ya mwisho. Atapigwa atolewe kutoka katika dhehebu nzima kwa jumla, na ndipo yale mavuno makuu yatakapokuwepo hapa. Hadi wakati huo, Bwana, wape afya na furaha wakutumikie Wewe. Katika Jina Lake Yesu. Amina.

> Nampenda, nam-(Je, mnampenda kweli?)
> Kwani alinipenda kwanza,
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

218 Na sasa mnaelewa kwa nini mimi huwakemea? Si kwa sababu nawapenda—ama kwa sababu siwapendi; nawapenda. Nataka Kipeo kwa ajili ya Bwana. Huenda ikanilazimu kurarua wachache na namna hii, bali nitapata Kipeo mojawapo ya siku hizi nikikiweka moja kwa moja katika Neno hili. Hiyo ni kweli.

219 Sasa, Yesu alisema, "Hivyo watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mkipendana ninyi kwa ninyi." Tunapaswa kupendana sana . . .

Kibarikiwe kifungo kinachoifunganisha
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa mioyo ya nia moja
Ni kama ule wa kule juu.

Hebu tupeane mikono.

Tunapoachana,
Tunapata maumivu ya moyo;
Bali tungali tumeungana moyoni,
Na kutarajia kukutana tena.

Peleka Jina la Yesu
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako.

Thamani, na tamu,
Ni Jina lake Yesu;
Thamani, na tamu,
Ni jina lake Yesu.

Sasa kumbuka katika safari yako:

Peleka Jina la Yesu
Liwe silaha zako;
Utakapojaribiwa (Utafanyaje basi?),
Lilia Jina hilo.

Loo! Thamani, na tamu
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu,
Ni Jina Lake Yesu.

Hata twonane (Hebu na tuviinamishe vichwa vyetu.) huko juu, (Loo, napenda kuimba!)
Hata twonane Kwake Kwema;
Hata twonane huko juu,
Mungu awe nanyi daima.

*Kile Kipeo* SWA64-0705
(The Masterpiece)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili, Julai 5, 1964, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2011.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org